# Nipashe

Jumamosi Agosti 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581029

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,019,301,493/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**CCM** yaagiza kupimwa maeneo huduma za kijamii

UKURASA 3



**KONATE KUKOSA MWANZO WA MSIMU**

UKURASA 22

# UGUMU WA MAISHA

• **Rais** Samia ataja hatua za kuwanusuru wananchi... *Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akizindua mradi wa maji safi wa Shongo-Mbalizi, katika eneo la Mbalizi, mkoani Mbeya jana. Wengine ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa tatu kulia), Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto) na wa pili kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. **PICHA: IKULU**

## EWURA yawatuliza wananchi bei mafuta

UKURASA 3



## Chalamila asimulia alivyoishi baada ya Samia kumtumbua

UKURASA 2


**MICHEZO** **YANGA SC: SIKU YETU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia ataja hatua za kukabili ugumu maisha

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali itaendelea kuchukua hatua zinazolenga kumlinda mwananchi dhidi ya upandaji wa gharama za maisha uliosababishwa na kupanda kwa bei ya mafuta duniani.

Mkuu wa Nchi huyo alitoa kauli hiyo jana alipohutubia wananchi njiani katika siku yake ya kwanza ya ziara ya siku tatu mkoani Mbeya.

Alisema moja ya hatua hizo ni kuweka ruzuku ya Sh. bilioni 100 ambayo kila mwezi serikali inaiweka kwenye mafuta.

Rais alisema Tanzania ilikuwa na tatizo la mafuta ya aina mbili, yakiwamo ya kupikia ambayo Waziri wa Kilimo amefanya kazi nzuri na sasa yameshuka bei.

Kuhusu mafuta kwa ajili ya magari na mitambo, Rais Samia alisema ni tatizo la dunia nzima, yanaendelea kupanda bei duniani.

"Hatua tuliyochukua kama serikali ni kutafuta ruzuku ya kushusha bei ya mafuta, tungeachia yapande bei kama yanavyokwenda duniani, leo yasingenunulika. Serikali inatoka Sh. bilioni 100 kila mwezi kutoa ruzuku kwenye mafuta bei zibaki zilipo.

"Suala la mafuta mpaka huko duniani waache kupigana, mpaka huko duniani waanze kushusha bei ndiyo tutapata unafuu, vinginevyo fedha mnazodai za barabara na umeme itabidi tukate tupeleke ruzuku kwenye mafuta kuzuia bei isipande," alisema.

Rais Samia alisema kwenye mafuta serikali ipo macho na inajua na inajitahidi isipande kwa kiasi kile kinachopanda kwa wengine.

"Ukichukulia bei ya mafuta kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna nchi ambazo mafuta hayanunuliki lakini marais wote tunajitahidi kila mmoja kwa njia yake kupunguza bei. Bei ya mafuta ni tatizo la ulimwengu mzima, tunajitahidi zibakie pale zilipo," alifafanua.

**MRADI WA MAJI**

Akizindua mradi wa maji wa Shongo-Mbalizi ulioko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani humo, Rais Samia aliwaagiza viongozi wa serikali kushirikiana na wananchi kuwashughulikia watu wote wanaoharibu vyanzo vya maji.

Alisema wananchi ndiyo walinzi wa kwanza wa vyanzo vya maji vilivyoko kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Nchi alisema kazi ya serikali ni kuyachukua maji kutoka kwenye chanzo kwenda kuwanufaisha wananchi na hivyo lazima kuwe na ushirikiano baina ya pande hizo mbili kwenye ulinzi wa vyanzo vya maji.

"Mkiona watu wanakwenda kuharibu chanzo cha maji, washughulikieni kwa mujibu wa sheria ndogo ambazo mmejiwekea kwa kushirikiana na halmashauri yenu, maji haya ni kwa faida yenu, serikali kazi yetu ni kuyatengenezea mfumo," aliagiza.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.3, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga, alisema umejengwa na wataalamu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya.

Alisema mradi huo wenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo milioni nne mpaka lita milioni 12 kwa siku, una mtandao wenye urefu wa zaidi ya kilomita 45 na kutoka kwenye chanzo mpaka kwenye tangi ni kilomita 15.

"Kwa sasa wanatumia lita milioni nane pekee kutokana na mahitaji. Hili tangi lina uwezo wa kuchukua lita za maji milioni 1.5 kwa siku na huu mradi unahudumia watu zaidi ya 80,000 wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi," alisema Sanga.

Alibainisha kuwa mradi huo umeongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka chini ya asilimia 50 mpaka kufikia asilimia 95 na Mji wa Mbalizi hauna tena tatizo la maji.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliishukuru serikali kwa kutekeleza mradi huo, akirejea hali ya awali kwamba wananchi wa Mji wa Mbalizi walikuwa wanapata shida kupata huduma hiyo.

Rais Samia anaendelea na ziara ya kikazi mkoani Mbeya ambapo leo atakuwa wilayani Chunya kabla ya kutembelea Halmashauri za Mbarali, Rungwe na Kyela.

**■Imeandaliwa na Nebart Msokwa na Grace Mwakalinga, (MBEYA) na Romana Mallya (DAR).**



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adamu Malima (katikati), akikagua shamba la karoti katika maonyesho ya wakulima Nanenane ya mikoa ya Kanda ya Magharibi, jijini Mwanza jana, huku akitoa maelekezo kwa wataalamu wa kilimo kuhakikisha zao hilo linalimwa katika ubora. **PICHA: ROSE JACOB**

# Jaji Mkuu apata dawa mlundikano mashauri

**Na Christina Haule, MOROGORO**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, amesema kuna haja ya kuweka utaratibu wa kila Jaji wa Mahakama ya Rufani kumaliza idadi fulani ya mashauri kwa mwaka ili kuondoa mlundikano wa mashauri mahakamani.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa mkutano wa nusu mwaka wa Majaji wa Mahakama ya Rufani uliofanyika mjini hapa, akibainisha kuwa mahakama haijaweka kiwango, bali unatumika utaratibu wao wa muda mrefu tangu mwaka 1979, yaani miaka 43 iliyopita.

Alisema, utaratibu huo hufanyika kila kinapoketi kikao cha Mahakama ya Rufani kinapaswa kumaliza mashauri yote yanayopangwa katika kikao husika isipokuwa kama kuna sababu zisizozuilika za kutokumaliza shauri husika ambapo pia hawakufikia malengo.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa Mahakama ya Rufani ina mashauri ya muda mrefu 611 na mashauri 42 yanayosubiri kusomwa hukumu yaliyozidi siku 90.

Alisema vigezo vya kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani vinalenga kushusha mlundikano hadi asilimia 0.05 ambapo tayari wamefanikiwa kushusha kwa asilimia 0.15 na kwamba lengo kuu ni shauri liwe mahakamani ndani ya siku 350.

Alisema wako vizuri katika kutekeleza hilo, sasa shauri linadumu mahakamani kwa wastani wa siku 338.

Jaji wa Mahakama ya Rufani, Augustine Mwaliga, alisema kikao hicho kimefanyika mwaka huu baada ya kutokufanyika kwa miaka miwili mfululizo iliyosababishwa na janga la UVIKO-19.

# Chalamila asimulia alivyoishi baada ya Samia kumtumbua

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, ameripoti kwenye ofisi yake mpya, akiwaomba wananchi wa mkoa huo 'kumwelewa'.

Amesema kuwa alipoondolewa madarakani na Rais Samia Suluhu Hassan, alikuwa katika kile alichokiita dunia yake mwenyewe na sasa amerudi na kupewa jukumu na Mkuu wa Nchi kusimamia mkoa huo.

Chalamila alitoa kauli hiyo juzi wakati wa makabidhiano ya ofisi na mtangulizi wake, Meja Jenerali Charles Mbuge, akiwaomba wananchi kumpa ushirikiano ili kusukuma mbele maendeleo.

Aliwaomba wananchi wa mkoa huo pamoja na viongozi kumwelewa na wasiotaka kumwelewa, wakae kimya.

Chalamila pia aliwataka watumishi kushirikiana na kuachana na tabia ya kuoneana katika fursa za uchumi.

Kiongozi huyo alisema wapo wafanyakazi wazuri na kuna kundi lingine la wanaofanya mzaha kwenye maeneo yao ya kazi.

"Wengine wapo kwa ajili ya 'jokes' (utani), wanaona kama haujafanya kazi. Mtu akijitoa akafanya kwa maendeleo ya wananchi, wengine watasema hajafanya chochote," alisema Chalamila.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema hakuna sababu ya kutotekeleza majukumu kwa kuwa mambo hayo yanakuwapo, hivyo ni muhimu kufanya kazi na kushirikiana.

"Mimi kwa mfano hapa mkuu wa mkoa inakuja OC (fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo), unauliza kiongozi wa idara hiyo sekretari alishawahi kula hiyo OC au alishawahi kuwa na ziara ya sekretari kwenda mahali.

"Wengine huwa mnaziona pesa tamu sana, lakini ujiulize falsafa ya hela unaweza kuchukua bure? Yaani inatengenezwa kwenye ulimwengu wa ajabu sana, inatakiwa ujenge tu busara, yaani inakonipeleka hii hapana!" Chalamila alisisitiza.

Chalamila aliwahi kushika nafasi hiyo katika mikoa ya Mbeya na Mwanza ambako, uteuzi wake ulitenguliwa muda mfupi baada ya kutoa kauli ya kuwaruhusu wananchi kuwa na mabango, yakiwamo ya kutukana wakati wa ziara ya Rais Samia mkoani humo.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Mbuge, alisema katika utumishi wake kwa nafasi hiyo alisimamia miradi ya maendeleo kwenye mkoa huo na ana imani itaendelezwa.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Toba Nguvilla, alisema amepata nafasi ya kutumika na ataitumia vizuri na kuwa tayari kupokea ushauri.

Alisema wapo viongozi ambao hupewa madaraka na kuvimba, kitu ambacho hakitakiwi kwa kiongozi anayetegemewa kuinua wananchi.

## HABARI KITAIFA

# EWURA yawatuliza wananchi bei mafuta

**Na Romana Mallya**

WAKATI ongezeko mfululizo la mafuta kwa Julai na Agosti likizua mjadala, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa ufafanuzi kuwa bei za Julai zilizoonekana kupungua zitatumika Septemba, mwaka huu.

Jumatano ya wiki hii, EWURA ilitangaza bei mpya za mafuta ambazo zitatumika mwezi huu zikionyesha kupanda kama zaidi kulinganisha na zile za Julai, kitendo ambacho wadau mbalimbali walitoa maoni wakiitaka serikali iangalie namna ya kudhibiti.

Katika mitandao ya kijamii, kumeibuka mijadala na maandiko vikiitaka EWURA kutoa ufafanuzi zaidi wa upandaji mfululizo wa bei za mafuta kwa miezi minne mfululizo huku wakienda mbali zaidi kutaka ieleze mafuta yanayopanda bei kwenye soko la dunia yanatoka kwenye soko gani.

Moja ya hoja iliyojengwa na wadau ambayo EWURA imeifafanua ni kwamba mara ya mwisho bei ya mafuta ilipanda Juni 5, mwaka huu, ambapo bei ya soko ambalo Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) iliwahi kusema inanunua kwa Dola 123.250 kwa pipa mafuta yasiyosafishwa. Kutoka mwezi huo, mafuta yameendelea kushuka na kuuzwa kwa wastani wa Dola 99 hadi 103 kwa pipa moja.

Wadau wanafafanua mitandaoni kwamba mafuta yalishuka hadi Dola 92 katika wiki ya kwanza ya Julai ikimaanisha kwamba hifadhi ya mafuta ambayo yalinunuliwa mwezi uliopita kwa matarajio ya kutumika Agosti, yangekuwa rahisi zaidi.

Nipashe ilipomtafuta jana Meneja wa Uhusiano na Mawasiliano wa EWURA, Titus Kaguo, ili kufafanua hoja hizo alisema vita vya Russia na Ukraine vilisababisha ongezeko kwa mahitaji ya soko la dunia kwa sababu Russia inachangia asilimia 10 ya mafuta yote duniani.

"Kwa mfano, bei za Agosti mafuta ya petroli yaliyosafirishwa yaliuzwa Dola 142.08 kwa pipa tofauti na ya Juni ambapo yaliuzwa Dola 119.18. Hii inaonyesha kwa kiwango gani bei zinapanda ukiachana na kupanda kwa soko la dunia.

"Pia gharama ya kukodisha meli imepanda baada ya Urusi (Russia) kuzuia meli zaidi ya 250 kufanyabiashara ya usafirishaji mafuta. Kumbuka kuwa Urusi ni moja ya nchi zenye usajili mkubwa wa meli za mafuta duniani," alisema.

Kaguo alisema pamoja na kupanda huko serikali imepunguza bei za mafuta ambapo Bandari ya Dar es Salaam, serikali imechangia Sh. 220 kwa kila lita ya petroli na kwa dizeli Sh. 412.

"Bandari ya Tanga serikali imechangia Sh. 149 kwa kila lita ya petroli na kwa dizeli Sh. 580. Bandari ya Mtwara serikali imechangia Sh. 367 kwa kila lita ya petroli na dizeli Sh. 582.43 ambapo jumla ya mchango wa serikali katika mafuta kwa mwezi Agosti ni Sh. bilioni 100."

Alisema bei katika soko la dunia za Juni 2022 ndizo zilizoleta bei za Agosti na zile za Julai zinazoonekana kupungua zitatumika Septemba.

"Kwa nini vita ya Urusi na Ukraine inatupiga? Ni kwa sababu Urusi huzalisha mapipa 10,778,00 kwa siku na Saudi Arabia huzalisha mapipa 10,835,00 kwa siku," alisema.

Jumatano ya wiki hii, EWURA ilitangaza bei mpya zitakazotumika mwezi huu wa Agosti ambapo katika Mkoa wa Dar es Salaam bei ya petroli ikilinganishwa na mwezi Julai, imepanda kwa Sh. 190 kwa kila lita, dizeli Sh. 179 na mafuta ya taa Sh. 323.

Kwa mujibu wa taarifa ya EWURA, bei ya rejareja mkoani humo kwa mafuta ya petroli kwa sasa inauzwa Sh. 3,410 kutoka Sh. 3,220 mwezi uliopita, dizeli Sh. 3,322 kutoka Sh. 3,143 na mafuta ya taa Sh. 3,765 kutoka Sh. 3,442 kwa lita.

## TEHAMA kuchangia 3% pato la taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC), imejipanga kuongeza mitandao ya dunia inayopita chini ya bahari ili kuchochea uchumi wa kidigitali.

Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza chachu kwenye uwekezaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) itakayochangia pato la taifa kwa asilimia tatu ifikapo mwaka 2025.

Mkurugenzi Mkuu wa ICTC, Nkundwe Mwasaga, akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema Tanzania ina sifa ambazo zinaifanya kuwa eneo muhimu la biashara za kikanda ikiwamo kuungana na nchi nyingi ambazo hazina nafasi ya kuunganisha mtandao kupitia bahari.

"Kwa sasa kuna mitandao mitatu, miwili inafanya kazi na mmoja unatarajiwa kuanza kufanya kazi, watu kama Rwanda, Burundi, Mashariki mwa Congo, Zambia, Malawi, Uganda, Msumbiji ili kuunganishwa na dunia lazima wapitie Tanzania," alisema. Mwasaga alisema mitandao hiyo ikiwa mingi gharama ya huduma itapungua.

"Uwekezaji huu lengo uongeze chachu ya kutengeneza kazi nyingi kwa kuwa katika uchumi wa dunia sekta ambazo zimejionesha wazi kwamba zinazalisha kazi nyingi ni TEHAMA.

"Kama mnavyofahamu ubunifu uliofanyika kupitia mitandao ya simu unasaidia watu kutuma fedha kwenda simu nyingine umezalisha kazi nyingi zamani hawa watu walikuwa wafanyakazi wa benki,"alisema.

Alisema kazi ya tume ni kuhakikisha inaleta uwekezaji mkubwa ili kuzalisha ajira nyingi zaidi.

"Tume inachokifanya ni kutengeneza kampuni nyingi za kitanzania ili zitengeneze huduma itakayotoka nje ya mipaka ya Tanzania kupitia mtandao uliopo, na kuvutia kampuni kubwa za TEHAMA kufungua ofisi zake Tanzania," alisema.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbroad Mtafungwa akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa ukaguzi wa mabasi ya shule, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## CCM yaagiza kupimwa maeneo huduma kijamii

**Na Mary Geofrey,** ROMBO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupima maeneo yote ya huduma za jamii na kutoa hati miliki ili kuepuka migogoro ya ardhi.

Chongolo alitoa agizo hilo jana wakati akikagua mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Mamsera wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro, akiwa ziarani kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhimiza ushiriki wa Sensa ya Watu na Makazi.

Alisema, maeneo mengi ya huduma za jamii yana migogoro kwa sababu ya serikali kutoyapima na kupatiwa hati miliki.

"Nitoe wito kwa TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, lazima sasa tuweke kipaumbele cha kupima maeneo ya huduma za jamii nchi nzima, tuwe na hati miliki ili yasiingiliwe na watu na tusiwe na migogoro isiyo ya lazima.

"Hapa kwenye mradi mmesema mmechukua eneo la shule na mengine mmenunua maeneo ya wananchi. Leo bila ya kuyapima na kukabidhi hati kwenye halmashauri, itatokea watoto au wajukuu kuja kusema tumeingilia 'kihamba' (eneo) letu na kwa sababu hela amechukua baba na hayupo, wajukuu wataanzisha mgogoro ambayo hatutaweza kuimaliza bila ya kuwa na hati," alitahadharisha.

Chongolo alisema, wizara inatakiwa kuweka mpango mkakati wa kupima kwa kipindi fulani kwa kuanza kuyatambua na kupima kwa idadi.

Alisema, maeneo yanayotakiwa kuwa na hati miliki ni viwanja vya michezo, maeneo ya shule, hospitali na huduma nyingine muhimu, akisema kinyume cha hivyo, yatakosekana maeneo ya kufanyia huduma za jamii.

Awali, Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Rombo, Petronilla Wakulila, akitoa taarifa ya ujenzi wa shule hiyo, alisema mradi huo unagharimu Sh. milioni 470 na ikiwa bado zinahitajika Sh. milioni 130 kuukamilisha na kuanza kutumiwa na wanafunzi.

Alisema, mradi huo ulianza Februari 25 mwaka huu na unahusisha madarasa nane, maabara tatu za sayansi, jengo la utawala, maktaba, matundu vya vyoo 20, na matangi ya maji lita 10,000.

"Uchelewaji wa kuanza mradi umesababishwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa eneo la wazi katika Kata ya Masera linalotosheleza ujenzi wa shule kubwa kama hii," alisema.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali Mstaafu Ngemela Lubinga, aliwataka wananchi wa Wilaya ya Rombo kuhifadhi chakula ili kuondokana na tatizo la njaa kwa siku za usoni.

"Duniani kote hali siyo njema, ili kuondokana na njaa ninaomba mtumie vizuri chakula mlichonacho kwa ajili ya kutunza familia," alishauri.

## Makada 94 CCM wajitosa uchaguzi Bunge A. Mashariki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JOTO la uchaguzi wa wabunge wa Afrika Mashariki limeendelea kupanda baada ya makada wengine 30 jana kujitosa kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwania nafasi hizo na kufikia 94.

Miongoni mwa makada hao ni waliowahi kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Bunge la Afrika Mashariki.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu wa NEC Oganaizesheni, Dk. Maudline Castico, alisema wanachama hao wamechukua fomu Makao Makuu ya CCM Dodoma, Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar na Ofisi Ndogo ya CCM Dar es Salaam.

Aliwataja wanachama hao ni Laurence Ngolly, Mona Mangula, Faraja Malaki, Nafue Nyage, Francis Songoro, James Millya, Theddy Patrick, Mhandisi Caroline Lyimo, Hamis Rajabu, Daudi Majinge, Methusela Mbajo, Crescentius Magori, Benedict Kikove, Mhandisi Frank Mejooli, Aloyce Mushi.

Wengine Comfort Maugo, Mussa Mgata, Doris Mollel, Julieth Rushuli, Alfred Elia, Alfred Sallwa, Gilbert Bankobeza, Doreen Noni, Deodatus Kinawiro, Shedrack Mashauri, Israel Ilunde, Machano Ali Machano, Rahma M. Ibrahim, Sabra Zubeir Said na Faki Ame Kesi.

Orodha hiyo pia ina majina ya waliochukua na kurejesha fomu: Nasikiwa Berya, Amina Mgeni, Ambwene Kajula, Nasser Nzamba, Prackseda Marmo, Maria Kangoye, Shogo Mlozi, Godfrey Shirima, DK Paul Anthony, Henry Bulengera, James Kasurura, Alfa Munyi, Manase Michael, Ayubu Lemilya, Nicksoni Kahimba na Mhandisi Haji Vuai Ussi.

Wanachama wengine ni Brigedia Jenerali mstaafu Marianus Mhagama, Mwanamanga Mwanduga, Conrad Lushakuzi, Balozi Anastase Rwegayura, Khadija Kayanda, Elibahati Lowassa, Masengwa Busigosolwe, Thomas Kitima, Reginald Shirima, Luvuva Salum Ali, Dk. Abdallah Hasnuu Makame na Mmanga Mjengo Mjawiri.

Wengine ni Jonas Lufungulo, Dk. Linda Salekwa, Loti Lembrice, Richard Mbuguni, Angela Kiza, Wakili Pascal Mayala, Francis Nanai, Melinda Muganda, Fikiri Luganga, Mkondo Fabian, Albert Mbago, Robison Etuttu na David Mwakanjuki.

Wengine ni Amani Kajuna, Azizi Mussa, Judith Mollel, Amedeus Mzee, Kalunde Malale na William Reuben, Fancy Khuni, Salma Mwassa, Ngwaru Maghembe, Happyness Lugiko, Shabu Makonyola, Salimu Kungulilo.

Wamo pia Prof. Norman Sigalla, Harrison Lukosi, Rehema Hassan, Ahmed Nkhuli, Steven Mkomwa, Dorica Gwilenza na Ansar Kachabwa, Nadra Juma Mohamed, Ahmed Shehe Saleh, Mar-yam Said Mussa na Mourie Oscar Sendera.

Katibu huyo wa NEC alitoa wito kwa wanachama wengine wenye nia, kujitokeza kuchukua fomu ili kuwania nafasi hizo ikiwa ni kutimiza takwa la kikatiba na uchukuaji huo utafungwa Agosti 10 mwaka huu.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula (kushoto), akikabidhi msaada wa fedha kwa Mwenyekiti wa wazee wa makazi ya Sukamahela, wilayani Manyoni, mkoani Singida, Andrea Yohana, alipowatembelea juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi mwingine kuzalisha MW 2,000 umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI serikali ikiendelea na utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa maji kwenye Mto Rufiji ili kuzalisha MW 2,115, neema nyingine imeishukia sekta ya nishati baada ya jana kutiwa saini mkataba wa kuzalisha MW 2,000 kwa kutumia nishati jadidifu.

Waziri ya Nishati, January Makamba, alisema juzi jijini Dar es Salaam kuwa mkataba wa makubaliano uliotiwa saini baina ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Masdar kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), utasaidia kuongeza uzalishaji wa kiwango hicho cha megawati za umeme zitakazoingizwa kwenye gridi ya taifa.

Alisema kwa uzalishaji huo wa umeme, uwezo wa Tanzania utaongezeka katika sekta ya nishati, kutokana na utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa umeme kwa njia ya maji kupitia Bwawa la Mwalimu Nyerere huko Rufiji.

Wakati wa utiwaji saini mkataba wa utayarishaji baina ya TANESCO na Masdar, Waziri Makamba alisema hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio yaliyoafikiwa wakati wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan katika Falme za Kiarabu Februari, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema baada ya hatua hiyo, kinachofuata ni kuanza utekelezaji wa mradi wa uzalishaji umeme utakaotokana na upepo, jua na joto ardhi.

Mwakilishi wa UAE, Abdulah Mohamed Abdulah Zayed, akizungumza kwa niaba ya kampuni ya Masdar, alisema nia ya kuingia makubaliano na TANESCO ni kusaidia upatikanji wa nishati ya umeme nchini kupitia njia mbadala kama jua, upepo na joto ardhi.

Alisema utekelezaji wa mradi huo utawezesha Tanzania kufikia uwezo wa MW 4,000 kutoka uwezo wa sasa ambao ni chini ya MW 2,000 na hivyo kuwezesha kuwa na umeme wa ziada utakaouzwa nje ya nchi.

Alibainisha kuwa kwa hatua ya awali ya utekelezaji wa mradi huo, wataanza na uzalishaji wa MW 570, na kiwango cha uzalishaji kitakuwa kinaongezeka hatua kwa hatua, uzalishaji umeme ukitarajiwa kuanza rasmi mapema mwaka 2024.

**KICHEKO GESI YA MAGARI**

Wakati neema hiyo ikitangazwa kwenye uzalishaji wa umeme nchini, kicheko kingine kwa Watanzania ni utatuzi wa kero ya uhaba wa vituo vya kujazia gesi kwa ajili ya magari yao, Kampuni ya GRAF Industries ikiahidi kuwekeza nchini ili kukidhi mahitaji ya nishati hiyo.

Kampuni hiyo kutoka Italia ilianza uzalishaji wa bidhaa zinazotumika katika usimikaji wa vituo vya gesi iliyosindikwa (CNG) na gesi iliyopo kwenye kimiminika (LNG) mwaka 1994 ikitoa huduma katika mataifa ya Misri, nchi za Umoja wa Ulaya, Urusi na Amerika ya Kati.

"Tunatafuta ubia na kampuni za ndani na tupo tayari kwa ajili ya kuwezesha ongezeko la vituo vya kujaza gesi katika magari (CNG). Tumeshawishika na mwenendo wa mahitaji kwa sasa Tanzania," Federico Soragni, Meneja wa Mauzo wa Kimataifa wa Kampuni hiyo, alisema jana Jijini Dar es Salaam.

Federico alitangaza neema hiyo wakati wa Kongamano la Kimataifa la Nishati 2022 lililofanyika kwa siku mbili kuanzia juzi kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, ikiwa ni mara ya nne kufanyika tangu kuanzishwa kwake mwaka 2017.

Licha ya Tanzania kuwa na kiwango kikubwa cha gesi tangu mwaka huu 2009, kuna vituo viwili tu vya kujaza CNG vilivyopo Ubungo chini ya Kampuni ya Uzalishaji Gesi ya PanAfrican Energy Tanzania (PAET) na kingine Tazara (vyote Dar es Salaam) chini ya Kampuni ya Enric Gas Technology Tanzania Limited.

"Tuko hapa kuhakikisha tunawezesha zaidi mahitaji ya vituo vya CNG na tumeona kuna mwitikio mkubwa wa sekta binafsi, bado hatujapata kampuni ya Kitanzania ya kushirikiana nayo lakini tunaamini tutafanikiwa," Federico alihitimisha.

# Kampuni kimataifa kuwekeza bandari, viwanda

**Mwandishi Wetu**

WAKATI Tanzania ikiendelea na juhudi za kuvutia uwekezaji kwenye sekta mbalimbali, kampuni mbili za kimataifa zinazojihusisha na uchukuzi na biashara zimetia saini makubaliano kuwekeza nchini.

Maeneo ya uwekezaji ni miundombinu ya reli, huduma za bandari, kongani za viwanda, huduma za kna shule ya ubaharia. Kampuni hizo ni AD Ports Group kutoka Abu Dhabi ambayo inajihusisha na huduma za uchukuzi kimataifa na Adani Ports and Special Economic Zone Ltd (APSEZ) ambayo inafanya shughuli zake nyingi nchini India, ambapo inaendeleza kuendesha bandari 12.

Kwa mujibu wa taarifa ya pamoja iliyotolewa na kampuni hizo juzi, kwa pamoja kampuni hizo zimekubalina kuwekeza nchini kutokana na fursa ilizopo hususan katika huduma za bandari na uchukuzi huku zikibainisha kuwa kwa siku zijazo Tanzania inaweza kuwa kitovu cha biashara barani Afrika.

Mkurugenzi Mkuu na Mtendaji Mkuu wa AD Ports Group, Kapteni Mohamed Juma Al Shamisi, alisema makubaliano yao na APSEZ yatazinufaisha kampuni zao kukua zaidi kimataifa, lakini zaidi ni manufaa kwa Tanzania kwa kuifanya kuwa kitovu cha biashara.

"Makubaliano haya uwekezaji ni muhimu kwa pande tatu. Kwanza, kuongeza uwezo na kasi ya Tanzania kuwa kitovu cha biashara katika Afrika na pia, kwetu sisi ni kukuza zaidi uwezo wetu wa kimataifa na miunganisho ambayo italeta bidhaa sokoni kwa haraka na kwa ufanisi zaidi," alisema Al Shamisi.

"Uwekezaji wetu wa kimkakati nchini Tanzania katika miundombinu na masuluhisho mbalimbali utawezesha makampuni ya kimataifa kuingia katika masoko ya Afrika. Sambamba na mwelekeo wa Uongozi wa Falme za Kiarabu (UAE), tunaiweka Abu Dhabi kwenye ramani ya magwiji wa kimataifa katika vifaa na viwanda," aliongeza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa APSEZ, Karan Adani, alisema: "Tunafurahi kushirikiana na AD Ports Group katika uundaji wa miundombinu muhimu ya ubora nchini Tanzania hasa katika sekta ya bandari, ambayo itaboresha na kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

"Tukisimama kwenye dhamira yetu ya ukuaji kwa wema. Tunaendelea kusaidia ajira za ndani, pamoja na ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa ujumla na nchi za Afrika Mashariki zitakazonufaika na uwekezaji wetu."

HABARI KITAIFA

## Chongolo: Sensa si ajenda ya kisiasa

**Na Mary Geofrey,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu, ni suala la kitaifa na siyo ajenda ya chama cha siasa au watu binafsi.

Amesema, sensa hiyo inahusisha Watanzania wote kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla na si vinginevyo.

Chongolo aliyasema hayo juzi katika shina namba mbili la balozi Kata ya Kaloleni wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro alipozungumza na wajumbe wa mashina na wanachama katika mwendelezo wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/25, miradi ya maendeleo na kuhimiza ushiriki wa Sensa ya Watu na Makazi.

Alisema suala hilo limegeuzwa kuwa ajenda za makundi ya watu binafsi wenye nia ovu ya kuchukulia kama suala linalowahusu wachache.

"Ninaomba niwaonye wana-CCM na wananchi, msidanganyike kuwa sensa ni ajenda ya kisiasa, bali ni jambo la kitaifa, kila mtu anatakiwa kushiriki kwa ajili ya kusaidia taifa kupanga maendeleo," alihimiza. Chongolo alisema, lengo ni kupata takwimu sahihi ili serikali itumie takwimu hizo kutoa miradi ya maendeleo kulingana na idadi kamili itakayopatikana.

Alisema, kama wananchi hawatajitokeza kuhesabiwa, watajipunja huduma muhimu wanazotakiwa kupata kutoka serikalini zinazoenda sambamba na idadi kamili ya watu.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti cha shukrani kwa Makamu wa Rais wa kampuni ya AngloGold Ashanti anayeshughulikia miradi endelevu Tanzania na Ghana, Simon Shayo, kwa niaba ya menejimenti ya kampuni ya AngloGold Ashanti Geita Gold Mining Ltd, waliopata tuzo hiyo kutokana na mchango wao kwa mwaka huu katika mkutano na maonyesho ya saba ya Wahandisi Wanawake Tanzania (TAWECE), jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa aipongeza GGML kwa kuwezesha wahandisi wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema serikali inatambua mchango wa wahandisi wanawake nchini, hivyo wajiandae kwa fursa na ajira mbalimbali zitakazotokana na miundombinu inayojengwa kwa wingi na serikali.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam hivi karibuni katika Kongamano la Saba la Wahandisi Wanawake Tanzania (TAWECE) lililoandaliwa na Taasisi ya Wahandisi Tanzania - Kitengo cha Wanawake na kudhaminiwa na Kampuni ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited.

Kongamano hilo kwa mwaka huu liliongozwa na kaulimbiu 'Uajirikaji, Uongozi na Ubunifu kwa Wahandisi Wanawake Tanzania'.

Majaliwa alisema, "Mpaka sasa, Tanzania tuna jumla ya wahandisi 30,921 ambapo wanawake ni 3,912, sawa na asilimia 12. Serikali imefanya uamuzi wa kujenga shule za ufundi wa kisayansi za wanawake katika kila mkoa ili kuongeza wanawake katika tasnia ya uhandisi."

Aliongeza kuwa serikali inajenga miundombinu wezeshi kuhudumia Watanzania, hivyo wahandisi wanawake wajiandae kwani fursa zipo na milango ya ajira iko wazi. "Wanawake mnaweza na wanawake wahandisi mnaweza zaidi! Nilipata fursa ya kutembelea Daraja la Tanzanite, ambapo mhandisi aliyetoa maelezo mwanzo mpaka mwisho alikuwa mwanamke. Mji wa Serikali Dodoma, mhandisi anayesimamia ujenzi wa mradi huo unaoendeshwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ni mwanamke. Mifano ipo mingi," alisema. Mbali na kuwapongeza wahandisi hao wanawake kwa ujenzi wa Shule ya Sekondari Kisarawe, alisema bado idadi ya wahandisi hairidhishi, hivyo jitihada zaidi zinahitajika kuhamasisha wasichana wengi wasome masomo ya sayansi.

Akizungumza katika kongamano hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema uhandisi kwa wanawake utaongezeka na kuimarika iwapo wahandisi wanawake wataendelea kushirikiana kuwahamasisha wenzao kujiunga kwenye uhandisi.

Mwenyekiti wa Kitengo cha Wahandisi Wanawake Tanzania, Upendo Haule, alisema wanawake ni viongozi mahiri na makini wakipewa fursa.

"Tunaomba serikali iendelee kuwapa fursa wahandisi wanawake ili waendelee kuliwakilisha vyema taifa la Tanzania," alisema Haule.

Baadhi ya wahandisi wanawake kutoka idara mbalimbali kwenye kampuni ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited pia walihudhuria kongamano hilo na kubainisha kuwa wanawake ni viongozi mahiri na makini wakipewa fursa.

Zuhura Khamis, mhandisi wa mifumo ya kampuni aliyehudhuria hafla hiyo kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, alisema ni jambo la kufurahisha kukutana na wahandisi wanawake wengi wenye vipaji.

Alitaja kuwa mapenzi yake katika somo la Hisabati, utatuzi wa matatizo na msukumo kutoka kwa mwalimu wake wa Hisabati wa shule ya msingi, ndiyo yaliyomjengea msingi wa taaluma yake kama mhandisi wa programu. Akizungumzia kizazi kijacho cha wahandisi wanawake, Zuhura alisema: "Ukiwa na malengo, inawezekana kabisa... Wasichana wasiogope kuwa wahandisi, inawezekana."

Katika kongamano hilo Waziri Mkuu alikabidhi cheti cha shukrani kwa Makamu wa Rais wa Kampuni ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited, Simon Shayo, na kuipongeza kampuni hiyo kwa kwa juhudi zake za kuwezesha ustawi wa wahandisi wanawake nchini, ikiwamo kudhamini kongamano kama mdhamini mkuu.

# Wabunge: Wateule wa Rais wapite mafunzo ya JKT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WABUNGE wameishauri serikali kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya awali ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa wakuu wa mikoa, wilaya na taasisi mbalimbali za umma ili kuwajengea uzalendo.

Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msavatavangu, alitoa rai hiyo jana aliposoma risala ya wahitimu mafunzo ya awali ya JKT, Operesheni Generali Venance Mabeyo, kundi maalum la wabunge na watumishi.

Alisema wanapendekeza serikali kutafuta mfumo ambao utatumika kwa wateule wa Rais kupatiwa mafunzo ya JKT, ili kuwasaida kuwa wazalendo kwa taifa lao na kufanya kazi kwa uadilifu.

"Tunapendekeza Bunge kuishauri serikali kuona namna ambayo mafunzo haya tuliyoyapata leo, iwe ni kitu cha muhimu kwa wateule wa Rais kukipata ili kuwasaidia kujifunza uzalendo na kulipenda taifa lao," alisema.

Aliiomba Ofisi ya Bunge kuendelea kutoa nafasi kwa wabunge wengine kushiriki mafunzo hayo ili kupata watu wengi ambao watakuwa na uzalendo kwa taifa lao.

"Tunatoa shukrani zetu kwa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uongozi wa JKT Makutupora kwa kutupatia fursa hii ya kushiriki mafunzo haya ambayo yametujengea uzalendo na kutufanya kuwa imara katika kutetea na kulinda taifa letu," alisema. Vilevile, mbunge huyo alisema wanaliomba Bunge kuishauri serikali kuanzisha vikundi rasmi vya vijana waliomaliza mafunzo ya JKT, ili kuwawezesha kufanya shughuli za uzalishaji mali.

"Tunaishauri serikali kuendelea kuboresha mazingira kwa kujenga miundombinu na kuweka vifaa vya kujifunzia katika kambi ili kutoa fursa kwa vijana wengi nchini kupata fursa hii ya mafunzo ya JKT," alishauri.

Mkuu wa Utumishi Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Meja Jenerali Paul Simuli, aliwataka wabunge hao kwenda kuisadia serikali kupinga vitendo vya uzembe kazini, rushwa na matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa.

"Ninapenda kuishukuru serikali yetu tukufu kwa kuendelea kuwezesha mafunzo haya kwa mujibu wa sheria. Mafunzo haya waheshimiwa wabunge yamewaongezea uzalendo, huko bungeni mtapokwenda mtakuwa wavumilivu na zile sarakasi bungeni ninatumai hazitakuwapo, pia hapa mmejifunza kufanya kazi kwa ushirikiano, hivyo mwende mkatekeleze majukumu yenu kwa ushirikiano," aliagiza. Pia aliwataka kutii kiapo walichoapa, akiagiza kila mmoja akaishi nacho moyoni mwake na kukitekeleza katika maeneo yao na bungeni.

Alitumia nafasi hiyo kuwataka Watanzania kuendelea kujilinda na maambukizo ya UVIKO-19.

Mkuu wa Kikosi cha JKT 834 Makutupora, Luteni Kanali Festo Mbanga, alisema kozi hiyo imepewa jina la Operesheni Generali Venance Mabeyo ili kuenzi kazi nzuri aliyoifanya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi mstaafu.

"Pia nitoe pongezi kwa wabunge na watumishi wa Bunge ambao wameshiriki kozi hii na kumaliza mafunzo na kufikia viwango licha ya kozi hii kufanyika kwa muda wa mwezi mmoja," alisema.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo yaliyoanza Julai 5 mwaka huu, yamesaidia kuwaongezea ari ya kufanya kazi zao bungeni na watumishi ambao wamehitimu kozi hiyo.

"Katika kozi hii tulikuwa na wanafunzi 39, ambao wote wamemaliza mafunzo, wabunge walikuwa 21 na watumishi wa bunge ni 18 ambao tumewafundisha uzalendo, ujasiri, stadi za kazi, usomaji ramani, ujanja wa porini, kufunga na kufungua silaha, mbinu za kivita, ushujaa, kwata, historia ya JKT na JWTZ," alisema. Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, alisema ofisi yake itaendelea kutoa fursa kwa wabunge na watumishi ambao watahitaji kupata mafunzo hayo kulingana na hali itavyoruhusu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi silaha muhimu vita vya ubingwa Ligi Kuu

**ZIKIWA** zimebakia siku 10 kuelekea kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu mpya wa mwaka 2022/2023, waamuzi wanaotarajiwa kuchezesha ligi hiyo ya juu nchini wamemaliza mafunzo yao.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kushirikiana na wakufunzi kutoka katika shirikisho la mchezo huo Afrika (CAF) na FIFA, hivi karibuni limemaliza semina za waamuzi kwa ajili ya kuchezesha ligi hiyo kwa weledi.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inadhaminiwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ndio inayotoa wawakilishi wa Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Kombe la Shirikisho Afrika, pamoja na michuano ya Kombe la FA.

Na sasa kwa msimu wa pili mfululizo, Tanzania Bara inawakilishwa na timu nne katika mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na CAF, hiyo imetokana na hatua nzuri iliyofikiwa na Simba kwenye michuano hiyo.

Waamuzi ambao wanakumbushwa kufuata weledi si wale wa Ligi Kuu Tanzania Bara pekee, hata wale wanaochezesha Kombe la FA kuanzia hatua ya awali, Ligi ya Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake Nchini.

Na kwa upande wa visiwani, Ligi Kuu Zanzibar na Kombe la ZFF ndio hutoa timu zinazoshiriki mashindano ya CAF, kila mwaka.

Ili ligi ipate bingwa wa nchi anayestahili au aliyetokana na ubora wa kikosi chake, ni lazima waamuzi wanaopewa dhamana wachezeshe mechi zote kwa kufuata sheria za mchezo huo unaopendwa zaidi duniani na si vinginevyo.

Waamuzi watakapopindisha sheria za mchezo huo, ni wazi timu zitakazotwaa ubingwa zitakuwa zisizostahili, lakini pia nchi itapeleka timu dhaifu kwenye mashindano ya kimataifa na matokeo yake wawakilishi hao watatupwa nje ya michuano hiyo mapema.

Umefika wakati waamuzi kuongeza umakini na weledi katika kutekeleza majukumu yao na kwa kufanya hivyo, itapunguza malalamiko na lawama mbalimbali kutoka kwa timu, wachezaji, viongozi na wadau wa michezo hapa nchini.

Mbali na kumaliza kero hiyo ambayo wakati mwingine inatafsiriwa inalenga kuzinufaisha baadhi ya timu, pia itawajengea sifa waamuzi kwa kupandishwa daraja na hatimaye kupangiwa mechi za kimataifa kama ambavyo kwa sasa mwamuzi msaidizi, Frank Komba anavyopata uteuzi wa michezo mbalimbali ya CAF.

Kuchezesha kwa haki kutawafanya wachezaji waendelee kujituma na kutokata tamaa hata pale wanapofungwa kwa sababu wanafahamu mchezo wa soka una matokeo ya aina tatu.

Haipendezi na haijengi katika dunia ya sasa ya utandawazi ambapo michezo yote 240 ya Ligi Kuu Tanzania Bara huonyeshwa mubashara, kama waamuzi watachezesha vibaya na hatimaye kupelekea kuvunjika kwa mechi au kutokea kwa vurugu.


Waamuzi wanapokuwa chanzo cha kutokea kwa matukio yasiyokuwa ya kimichezo au ya utovu wa nidhamu yanapunguza heshima ya maofisa hao, lakini pia huwanyima haki wale waliostahili kupata ushindi katika mechi husika.

Tunaamini semina ambazo TFF imewaandalia waamuzi zitazaa matunda na msimu mpya wadau watashuhudia burudani na si mauzauza ambayo yamewahi kutokea katika miaka ya nyuma.

Klabu zimesajili wachezaji wenye viwango vya juu kutoka sehemu mbalimbali, hivyo wanahitaji kuona haki inatendeka lakini pia tunasaidia kuwaimarisha na wanapoitwa kwenye timu za Taifa, wanakuwa imara na tayari kushindana na si kutegemea kufunga mabao kwa njia za ujanja ujanja.

Kila la kheri timu zote zinazotarajia kuchuana katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League, Ligi Kuu ya Wanawake Nchini, Kombe la FA, Ligi Kuu Zanzibar , Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar na mashindano ya Kombe la ZFF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mchakato matumizi VAR Tanzania ufanyike haraka

**UKIANGALIA** usajili uliofanywa na timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya msimu mpya, unakubali kuwa ligi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani.

Ligi itakuwa ngumu kuliko msimu uliopita, ambao wachambuzi wa masuala ya michezo wanasema ulikuwa mgumu pia.

Inavyoonekana ni kila msimu unaofuata kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, unakuwa mgumu zaidi kuliko uliopita.

Hii ni kutokana na klabu zinavyojipanga, kuanzia kwenye usajili hadi maandalizi.

Ukitaka kujua klabu zimejipanga kwa ajili ya msimu ujao, anza kwa kuziangalia timu ambazo hapo awali zilikuwa hazisajili wachezaji kutoka nje ya nchi.

Awali ilikuwamo Mtibwa Sugar, lakini kwa misimu miwili iliyopita iliondoka huko, ikaanza kusajili wageni, japo haikufanya vyema sana.

Klabu za majeshi kama Tanzania Prisons na Polisi Tanzania, lakini safari hii zimeamua kuingia huko huko. Zinaona kama zinaachwa nyuma na zinabaki kuhangaika tu kwenye ligi.

Kwa mara ya kwanza Polisi Tanzania imemsajili mchezaji raia wa Uganda, Ambose Awio, katika kile kinachoonyesha hali imeshakuwa ngumu ni lazima sasa zishindane na klabu nyingine, vinginevyo zinaweza kuachwa mbali.

Prisons nayo katika usajili wake pia imesema itasajili wachezaji watatu kutoka Kenya. Hii si hali ya kawaida kwa klabu za Tanzania, si ndogo tu, bali hata za Taasisi za Majeshi.

Hii inaonyesha timu hizo nazo zinataka wachezaji wenye viwango vya juu zaidi ili kukabiliana na ushindani mkubwa kutoka kwa vigogo wa soka nchini, Simba, Yanga na Azam, ambazo zenyewe ni jambo la kawaida tu kushusha wachezaji zaidi ya 10 kutoka nje ya nchi.

Kwa ujumla ni kwamba zinataka kuleta ushindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Kwa maana hiyo ni lazima kuwa na uwiano mzuri kwenye uamuzi.

Kwa miaka kadhaa tumeona klabu za Simba na Yanga ambazo zinakuwa na wachezaji wenye viwango vya hali ya juu kuliko timu nyingine, lakini pamoja na hayo zinanufaika sana na makosa yanayoitwa ya kibinadamu ya waamuzi wetu nchini.

Ni makosa ambayo yanaziadhibu timu ambazo zinajikongoja kusajili wachezaji kwa gharama ndogo na uwezo wa kawaida, lakini pamoja na kujitutumua na kuleta ushindani wa kweli, wanajikuta wanaangushwa na maamuzi hayo.

Hivi karibuni, tumeona kwenye Uwanja wa Azam Complex, waamuzi wakitumia mfumo wa uamuzi wa video (VAR), kwenye Ligi ya Vijana chini ya miaka 20.

Mashabiki wengi walifurahishwa sana na jinsi ilivyotumiwa kwa ufanisi kiasi cha kupendekeza itumike pia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati wa kutangaza ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Ofisa Mtendaji Mkuu, Almasi Kasongo, pamoja na mambo mengine alisema kwa msimu huu haitowezekana kwa sababu ni lazima kwanza jambo hilo liingie kwenye mchakato.

"Kwenye mashindano ya U20 tulianza na mfumo huo wa VAR uliokuwa umefungwa na wamiliki wa Uwanja wa Azam Complex na kuwa wa mafanikio makubwa, lakini mimi kama Mtendaji Mkuu ni lazima niseme jambo hilo bado linahitaji mchakato mrefu. Tumefanya majaribio kwa vijana, tumewasiliana na wataalamu wa CAF na FIFA, tumewaambia kama tuna kitu kama hiki, wao baadaye wamesema watatuletea wataalamu ili kuja kutazama na kuthibitisha, kama ukikamilika na kuthibitishwa basi hatutosita kuuingiza kwenye mpango wa waamuzi wetu kuwasaidia kwenye kutafsiri sheria," alisema Kasongo.

Kwanza kabisa niwapongeze Bodi ya Ligi kwa kuwasiliana na CAF na FIFA kuwaambia Tanzania tumefikia hatua hii ya kutengeneza VAR yetu.

Inaonyesha ilikuwa na nia ya dhati itumike msimu huu, lakini sasa itabidi tusubiri wakubwa CAF na FIFA waje kuthibitisha.

Nawashauri tu Bodi ya Ligi wawe wanawakumbusha mara kwa mara ili waje kuitazama, angalau msimu ujao tuanze kuwa na VAR.

Inawezekana ikianza kutumika, yale mambo ya makosa ya kibinadamu yatapungua sana kwa sababu refa atakuwa na fursa ya kwenda tena kuangalia nini kimetokea, kabla ya kurekebisha au kuendelea na uamuzi wake.

Kwa jinsi timu zilivyosajili imefikia wakati sasa zishinde kwa uwezo wao na si uamuzi mbovu wa waamuzi.

Klabu zinatumia gharama kubwa sana kusajili na kuweka wachezaji kambini, lakini zinakuja kukatishwa tamaa na maamuzi yasiyo sahihi.

Mchakato wa VAR unahitajika uharakishwe ili kila timu ishinde kwa uwezo wake, na mashine hiyo ndiyo mwarobaini wa yote.

# COSTECH yamwezesha mbunifu uzalishaji umeme

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imetoa msaada wa mashine ya kuchonga vipuri na kukata vyuma yenye thamani ya Sh. milioni 25 kwa mbunifu John Fute aliyejitengenezea umeme wake mwenyewe kupitia maporomoko ya maji.

Baada ya kukabidhi mashine hiyo juzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Ofisa Uratibu wa Utafiti COSTECH, Emmanuel Girimwa, alisema kazi ya tume hiyo ni kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali nchini, hivyo vijana wajitokeze kupata ujuzi kupitia karakana hiyo.

Girimwa alisema mbali na kununua mashine hizo kwa ajili ya kuiendeleza karakana hiyo, pia wametoa Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya gharama za uendeshaji ikiwamo ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kujikinga.

"Karakana hii inaweza kuhudumia zaidi ya vijana 100 na kwa bahati nzuri mzee ana eneo kubwa la kutosha kujumuisha vijana wengi kwa wakati mmoja," alisifu Girimwa.

Mbunifu Fute alisema kuwa kupitia msaada huo, sasa anawakaribisha vijana wa nyanda za juu kusini kujifunza kuunda pampu za kupandisha maji, uchongaji wa vipuri na nyenzo mbalimbali za kilimo.

Alisema vijana wengi wamejiajiri kwenye kuendesha pikipiki za kubeba abiria, maarufu bodaboda lakini zipo fursa nyingi ambazo wanaweza kuzipata endapo wataamua kujifunza masuala mbalimbali ya ufundi na ubunifu.

Alisema miongoni mwa fursa zilizopo ni utengenezaji wa vifaa maalum kwa ajili ya kuvuna chai na kuchuma parachichi, hivyo mashine hizo zitakwenda kuleta mapinduzi makubwa.

"Wabunifu wote ninawakaribisha mje tushirikiane kujifunza bure kwani nchi bila ya teknolojia hatuwezi kwenda popote," alisema Fute.

Aliiomba serikali kuwekeza kwenye ubunifu na wabunifu wenyewe ili kuwavutia wengine kuipenda kazi hiyo na kuahidi kufanya kazi kwa nguvu zote ili kuwasaidia vijana wenye ubunifu nchini. Baadhi ya vijana wanapata mafunzo kwenye karakana hiyo, wakiwamo Kelvin Kimaro na Abely Hongoli, waliishukuru serikali kwa kutoa mashine hiyo, wakiamini itawarahisha kazi.

"Tulikuwa tunapata tabu kwenda mbali kuchonga vyuma lakini kwa sasa mashine ipo, hivyo mmeturahisishia kwenye kazi zetu," alipongeza Hongoli.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo, Lariba na wakulima wa Benki ya NBC, Raymond Urassa (kushoto), akitoa maelezo kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa tatu kushoto), kuhusu huduma mbalimbali mahususi kwa wakulima zinazotolewa na benki hiyo, alipotembelea Maonyesho ya Wakulima Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika Uwanja wa John Mwakangale, jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa ataja vipaumbele ujenzi

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema vipaumbele vya wizara kwa mwaka wa fedha 2022/23 vinakusudia kuhuisha uchumi wa nchi na kuwakomboa Watanzania wa ngazi zote.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, huku akivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kukamilisha ujenzi wa barabara za lami zinazounganisha mikoa yote nchini ili kurahisisha huduma za usafiri na uchukuzi katika sekta mtambuka.

Vingine ni ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi lenye urefu wa kilomita 3.2 mkoani Mwanza, kukamilisha daraja la Wami linalounganisha mikoa ya Pwani na Tanga, ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano na magari yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam na barabara za mzunguko jijini Dodoma.

Prof. Mbarawa alisema serikali pia itaendelea na upanuzi wa bandari za Dar es Salaam na Tanga, ujenzi wa meli katika Ziwa Victoria na Tanganyika, upanuzi wa viwanja vya ndege na ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi wa umma katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tumejipanga kuhakikisha miradi hii tunayoitekeleza inazingatia thamani ya fedha na kuzalisha ajira kwa Watanzania wenzetu kadri inavyowezekana," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imejipanga pia kuhakikisha inawezesha wakandarasi wazawa na wahandisi wanawake kupata kazi na utaalam ili kuwawezesha kushiriki na kuendeleza kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa nchi.

Kuhusu maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) sehemu ya kwanza inayoanzia Dar es Salaam hadi Morogoro (kilomita 300), Mbarawa alisema majaribio ya reli hiyo yanatarajiwa kuanza Septemba, mwaka huu.

Kuhusu upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Prof. Mbarawa alisema ujenzi wa gati namba nane hadi 11 unaenda sambamba na upanuzi wa gati namba moja hadi mbili katika Bandari ya Tanga ili kuziwezesha bandari hizo kufanya kazi kwa ufanisi.

Waziri Mbarawa alisema Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaendelea kujenga mizani ya kisasa ili kudhibiti magari yanayozidisha uzito ili kuilinda miundominu ya barabara.

"Zaidi ya kilomita 500 za barabara za lami pamoja na madaraja makubwa manne yanaendelea kujengwa, wakati katika sekta ya uchukuzi ujenzi wa njia ya reli kipande cha Tabora - Isaka km. 165 na Tabora - Kigoma km. 411 zinatarajiwa kuanza ujenzi wake," alisema.

# Mashahidi 10 kujenga hoja kesi wizi mil. 505/- mafuta

**Na Grace Gurisha**

MASHAHIDI 14 wanatarajia kutoa ushahidi dhidi ya Meneja wa Kituo cha Mafuta cha GPB Tanzania Ltd, Uwanja wa Ndege Jijini Dar es Salaam, Mohamed Nassoro, anayedaiwa kuiba zaidi ya Sh. milioni 504.

Taarifa hiyo ya mashahidi na vielelezo tisa, ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Yusuph Aboud, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Pamela Mazengo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baada ya kumaliza kumsomea maelezo ya awali mshtakiwa huyo.

Aboud, akisoma maelezo hayo, alidai kuwa kati ya Mei Mosi na Oktoba 21, 2018 mshitakiwa akiwa maeneo ya Uwanja wa Ndege akiendelea na majukumu yake, aliiba Sh. 504,053,778 mali ya mwajiri wake, GPB Tanzania Ltd.

Alidai kuwa mshitakiwa aliaminiwa na kampuni hiyo akapewa fedha hizo ili akaziweke katika akaunti ya GPB iliyopo katika benki ya Equity lakini hakufanya hivyo kama alivyoelekezwa.

Wakili huyo alidai kuwa mshitakiwa alikamatwa na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi na kuhojiwa kuhusiana na tuhuma zinazomkabili kisha akapelekwa mahakamani. Baada ya kusomewa maelezo hayo, Hakimu Mazengo alimwuliza mshitakiwa kwamba anakubali yapi na anakataa yapi na kudai kuwa siku hiyo alikuwapo kazini na ni kweli yeye ni Meneja wa GPB.

Kuhusiana na wizi wa fedha hizo, Nassoro alikataa tuhuma hizo ndipo Wakili Aboud akaieleza mahakama kuwa watakuwa na mashahidi 14 na vielelezo tisa na pia wanaomba tarehe ya usikilizwaji.

Hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 18, mwaka huu, kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa mashtaka.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alirudishwa maabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana likiwemo kuweka mahakamani Sh 252,026,890. Pamoja na mdhamini mmoja atakayetia saini bondi ya kiasi hicho cha fedha.

# TAKUKURU yajipanga upya kuzuia rushwa

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imesema kuwa imeandaa kampeni mbili za kuzuia rushwa zinazojulikana kama 'Tusirudishane Nyuma Maendeleo Yako Maendeleo Yangu' na 'TAKUKURU Rafiki' kwa kuwashirikisha na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa miradi wanayopelekewa maeneo yao.

Lengo ni kuwafanya watambue maeneo yenye viashiria vya rushwa na kutoa taarifa mapema.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, jijini Dar es Salaam, alipohojiwa na Televisheni ya Taifa (TBC), kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa.

"Ni mkakati wa kuwaelimisha wananchi ili waone kuwa miradi inayopelekwa ni kwa ajili ya kuwasogezea huduma za msingi na kuwaletea maendeleo. Kwa hiyo mtu yeyote anayecheza na mradi basi watupe taarifa za mapema," alisema.

Hamduni alisema mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu la Watanzania wote, watimize wajibu wao kwa kutoa taarifa za wanaojihusisha na rushwa ili kurahisisha mifumo ya kisheria kama kufanya uchunguzi, kuendesha mashtaka na utaratibu wa kisheria wa kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia za rushwa na kumfunga mhusika.

Kuhusu usalama kwa watoa taarifa, Mkurugenzi huyo alisema kuwa zipo taratibu za ndani za kuwalinda ikiwamo mifumo ya kutuma taarifa bila kukutana na mtu kama vile barua pepe za wakurugenzi na mfumo wa kupiga simu wa 113.

"Ukimshughulikia kwa maana ya kumshtaki na kumfunga bila kufuatilia mazalia ya rushwa hato feel ile impact (hatoona uchungu), kwa hiyo sisi tunachokifanya kama tumeshindwa kuzuia vitendo vya rushwa vikajitokeza tunafanya uchunguzi ambao unaenda sambamba na ufuatiliaji wa mali," alisema Hamduni.

Alisema katika kuzuia vitendo vya rushwa wanafanya utafiti wa mifumo katika maeneo yanayotolewa huduma pamoja na kufuatilia matumizi ya fedha za utekelezaji wa miradi yote ya serikali ikiwamo iliyolenga kuwasogezea wananchi huduma za msingi ili kubaini kasoro na kutoa ushauri wa kuzirekebisha kabla tatizo halijatokea.

Alisema pia ofisi yake inapokea kero ndogo na kubwa za rushwa, ikiwamo kutoka vituo vinavyotoa huduma za kijamii kama vile hospitali, polisi, barabarani, halmashauri na ardhi na kuzifanyia kazi na kuwapa mrejesho.

Alisema, moja ya mambo yanayosababisha kuwapo kwa vitendo vya rushwa ni ukosefu wa maadili sehemu mbalimbali, ikiwamo kazini kwa kuwa jamii inawaona watu wanaofanya kazi kwa kufuata maadili kuwa hawafai na wale wabadhirifu na wezi wa mali ya umma kuwa ni wajanja.

Katika kupambana na hilo wameanzisha mkakati wa kuimarisha na kuboresha klabu za wapinga rushwa ikiwamo Skauti ili kujenga kizazi chenye maadili na uzalendo hapo baadaye kwa kuwa hao ndiyo wawajibikaji wa kesho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wajibu, Ludovic Utouh, alisema kuwa nchi imepiga hatua kubwa kupambana na rushwa ikilinganishwa na kipindi cha nyuma nao sasa hakuna matukio makubwa.

Aliyataja ni ubadhilifu wa fedha za madeni ya nje (EPA) na mamilioni ya dola kutoka kwenye akaunti ya Benki Kuu zilizohifadhiwa kutokana na mgogoro baina ya kampuni ya IPTL na Shirika la Kuzalisha na Kusambaza Umeme Tanzania (Tanzania) (ESCRO), kutokana na kuimarishwa kwa mifumo ikiwamo ya kisheria na kutolewa elimu kwa jamii.

Utouh aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alisema pia kinachoshangia kuwapo vitendo hivyo ni mfumo wa maisha ya ushindani wa matumizi waliojijengea Watanzania hali inayowasukuma kutafuta pesa kwa njia isiyo halali ili jamii iwaone kuwa wana maisha ya ufahari kuliko wengine.




Mkuu wa shule ya Hazina ya Magomeni, Dar es Salaam, Omar Juma, akimpa zawadi mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo, Iptusm Ramadhani, baada ya kuwa wa kwanza kwenye mtihani wa utamilifu shuleni hapo jana. Mtihani huo, ulifanyika hivi karibuni na shule hiyo kufanikiwa kuwa ya kwanza kwa Wilaya ya Kinondoni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wafugaji wataka maofisa ugani kufanya kazi karibu

**Na Mbaraka Kambona,** ARUSHA

WAFUGAJI katika Kanda ya Kaskazini, wameiomba serikali kuhakikisha maofisa ugani wanawafikia wafugaji kwa urahisi ili kuwapatia huduma stahiki wakati wote ili shughuli zao hizo ziwe na ubora na zenye tija.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Kaskazini yanayofanyika mkoani hapa, wafugaji hao walisema ni muhimu maofisa ugani wakawatembelea kila wakati na kutatua changamoto zinazowakabili.

Kwa mujibu wa wafugaji hao, kufanya hivyo kutasaidia kuboresha ufugaji wao na manufaa ya kazi hiyo yataonekana.

Mfugaji kutoka Arusha, Desderi Kimario, alisema wanahitaji maofisa ugani wa kilimo na mifugo wote kwa pamoja wawe wanafanya kazi karibu na wafugaji ili kuwawezesha (wafugaji) kufanya shughuli zao kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu hao na kufanya ufugaji wao uwe na tija kubwa kwao na nchi kwa ujumla.

"Tunaomba maofisa ugani wawe wanatutembelea mara kwa mara sisi wafugaji wadogo wadogo katika maeneo yetu huku kwenye kata na vijijini ili kujua matatizo yetu na si mpaka tufike kwenye maonyesho kama hivi. Maonyesho huwa ni mara moja kwa kila mwaka," alisema Kimario.

Naye Lawrence Kimambi, mfugaji kutoka Kilimanjaro, alisema kwa sasa ardhi imekuwa finyu, hivyo ni muhimu wafugaji waendelea kupatiwa elimu ya kulima malisho ya mifugo ili kuokoa changamoto ya malisho na kuleta manufaa zaidi kwa jamii za wafugaji na nchi kwa ujumla.

Naye Kelvin Manase kutoka Arusha alisema kama wafugaji wataendelea kuelimishwa vizuri kuhusu umuhimu wa ulimaji wa malisho ya mifugo, muda si mrefu migogoro kati ya wakulima na wafugaji itakwisha.

Ofisa Mifugo Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo, Israel Kilonzo, aliwashauri wafugaji hao kuanza kujifunza namna ya kustawisha malisho ya mifugo na kuachana na tabia ya kutegemea malisho ya asili peke yake kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza migogoro ya ardhi.

"Kama tunavyojua watu waongezeka na mifugo pia inaongezeka na ardhi iliyopo haitoshi kufanya ufugaji wa kuhamahama. Ni lazima tujifunze kustawisha malisho katika maeneo yetu na tujifunze kuyatumia vizuri ikiwamo kuwa na mifugo tutakayoimudu kuihudumia," alisema Kilonzo.

## Shule Hazina yazidi kung'ara mitihani Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Hazina ya Magomeni, Dar es Salaam, imeongoza kwenye matokeo ya mtihani wa utamilifu (Mock), darasa la saba kwa wilaya ya Kinondoni.

Kwenye matokeo hayo yaliyotolewa na Mkoa wa Dar es Salaam hivi karibuni, shule hiyo imeshika nafasi ya kwanza kati ya shule 158.

Mkuu wa Shule hiyo, Omar Juma, alisema jana kuwa Hazina iliongoza kwenye mtihani uliofanyika Aprili na ule uliofanyika Juni, mwaka huu.

Alisema walimu wake wamekuwa wakijituma kuwaandaa wanafunzi hao kwa ajili ya mitihani ya ndani na ile ya kitaifa na kwamba hiyo ndiyo imekuwa siri kubwa ya mafanikio kwao.

Alisema kutokana na maandalizi mazuri waliyoyafanya kwa wanafunzi hao wanaimani kwamba watafanya vizuri zaidi pia kwenye mtihani wa kitaifa wa darasa la saba mwaka huu.

"Sisi tunapiga kazi hapa ni kazi tu nawashukuru walimu kwa kuifanya shule hii kuongoza mtihani wa utamilifu kwa mara ya pili mfululizo hii inatupa moyo wa kuendelea kufanyakazi," alisema Omar. Alisema kujituma kwa walimu na ushirikiano ambao wamekuwa wakiupata kwa uongozi wa shule na wanafunzi ndiyo kitu wanachojivunia.

"Walimu wanafanya kazi kwa moyo sana, wazazi wa wanafunzi wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri sana kwa shule na uongozi wa shule unawajali sana walimu, hayo kwa pamoja yamekuwa yakisaidia ufaulu wetu kuwa juu mwaka hadi mwaka," alisema.

Aliwapongeza wanafunzi kwa mafanikio hayo na kuwataka wasome kwa bidii ili hatimaye waweze kuendelea kuongoza kitaifa na Mkoa wa Dar es Salaam kwenye mitihani ijayo.



## HABARI DODOMA

# NBC yahimiza wateja kukata bima biashara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya NBC imewataka wafanyabiashara kukata bima ya biashara ambayo itawasaidia wakati maafa yanapotokea.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa NBC, Mussa Mwinyidaho, alitoa ushauri huo juzi kwenye chakula cha jioni kwa wamiliki wa biashara wa Mkoa wa Dodoma kilichoandaliwa na benki hiyo ili kuongeza ukaribu na wateja wao.

Katika kikao hicho, NBC iliwafundisha wajasiriamali waliohudhuria na kuwapa vidokezo kuhusu jinsi ya kuboresha biashara zao na kukatia bima.

Aidha, alisema miongoni mwa bidhaa zinazotolewa na benki hiyo ni mikopo ya kuongeza mtaji unaojumuisha fedha za wasambazaji, dhamana ya utendaji kazi, dhamana ya malipo ya awali, mikopo ya uwekezaji na mikopo ya ujenzi wa majengo ya biashara.

Naye Mjumbe wa Bodi ya benki hiyo, Kassim Hussein, alisema ni muhimu kwa wajasiriamali kuwa na ujuzi na ufanisi wa kutumia huduma za kibenki na wawe na uaminifu kwenye kurudisha mikopo, na watumiapo huduma nyingine za kibenki.

Alisema, wajasiriamali wanatakiwa wawe wabunifu sana na wajitangaze ili kutengeneza wigo mpana wa kupata wateja wengi zaidi na kuongeza kipato kutokana na biashara zao.

Benki ya NBC, ilishinda tuzo kama taasisi bora zaidi ya kifedha inayosaidia wajasiriamali kwa mwaka 2018, na hivyo kuifanya kuboresha bidhaa na huduma zinazolenga kusaidia wajasiriamali kukuza biashara zao.

# TCDC kusajili wanachama kwa mfumo wa kidigitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) inatarajia kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa kusajili wanachama kwenye vyama vya ushirika ili kuondokana na kero zinazoikabili sekta hiyo nchini.

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga, alibainisha hayo jana kwenye maonyesho ya Nanenane Kanda ya Kati yanayofanyika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.

Alisema lengo la kusajili vyama na wanachama kwa njia ya kielektroniki ni kuongeza usimamizi, uwazi na kudhibiti vyama hivyo.

"Ushirika ni sehemu inayowanufaisha wananchi katika shughuli zao za kilimo, uvuvi na mifugo kwa kutambulika na kulinda maslahi ya wananchi kwa kuwasajili kidigitali ili mchango wao katika maendeleo ya nchi uweze kufahamika," alisema Nyakunga.

Hata hivyo, alisema kulikuwa na tatizo la kuwafikia wanachama kwenye vyama, hivyo kufanya ukaguzi kuwa mgumu.

"Maofisa ushirika waliopo si wengi lakini sasa tutavifikia vyama kupitia mfumo wa kielektroniki na kuvikagua kirahisi na vitatambulika na itakuwa rahisi kufahamu mchango wa ushirika katika pato la taifa na hakutakuwa na ugumu kupata takwimu na taarifa za ushirika," alisema.

Alisema, kwenye ushirika kuna manufaa makubwa tofauti na mvuvi, mfugaji au mkulima akiwa peke yake kwa kuwa hatapata nguvu ya soko la bidhaa zake.

Naibu Mrajis huyo alisema, awali zao la Kakao kilo moja ilikuwa linanunuliwa kwa Sh.1,800 lakini mara baada ya kuanza kuuzwa kupitia mfumo wa ushirika, bei imepanda hadi kufika zaidi ya Sh. 5,000.

"Miaka ya nyuma, kwenye korosho kulikuwa na udanganyifu wa vipimo na bei ilikuwa ndogo sana, lakini baada ya mfumo wa Ushirika kuanza kutumika sasa bei ni zaidi ya Sh. 1,600, Sh.2,000 hadi Sh.3,000 kwa kilo moja, haya ndiyo manufaa ya ushirika," alisema.



Askari polisi mstaafu wa Kikosi cha Reli nchini, Severini Ngumba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari Jijini Dodoma juzi, kwa niaba ya wenzake 60, kuhusu madai yao ya stahiki za posho za kujikimu za zaidi ya Sh. Bilioni moja, wanazolidai Shirika la Reli Tanzania(TRC), ambazo walitakiwa kulipwa wakati wa utumishi wao. Wengine, ni Enock Mpilimi (kushoto) na Michael Ngongi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askari wastaafu wa reli walilia mafao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ZAIDI ya askari polisi wastaafu 60, wa kikosi cha Reli Tanzania wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuwasaidia kulipwa posho zao za kujikimu zaidi ya Sh. bilioni moja wanazolidai Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Akizungumza jana katika ofisi za IPP jijini hapa, mmoja wa askari hao, Sajini Mstaafu Severine Ngumba, alisema hadi sasa wamefanya kila jitihada kufuatilia malipo yao bila mafanikio kwa zaidi ya miaka kumi sasa.

Ngumba alisema, kutokana na hali hiyo maisha yao na familia zao yamekuwa ya shida kwakuwa wameshindwa kumudu gharama za maisha ikiwamo ada kwa ajili ya watoto wao waliopo shule.

Alisema fedha anazodai ni posho za kujikimu ambazo walizifanyia kazi walipokuwa watumishi katika kikosi hicho ambapo walikuwa wakisindikiza treni za mizigo kwenda katika mikoa mbalimbali nchini.

"Mimi nimefanya kazi katika kikosi cha reli kwa miaka 21 na kazi ambazo tulikuwa tunazifanya ni kusindikiza treni ya mizigo ili kulinda watu na mali zao, kutoka Dar es Saalam kwenda Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Sinyanga, Mwanza Kigoma hadi Mpanda lakini tulikuwa hatulipwi na kama ukihoji tulikuwa tunawekwa mahabusu kwa madai kuwa tumegomea amri ya jeshi," alisema Ngumba.

Pia alisema, wamejaribu kudai malipo hayo ya posho za kujikimu lakini kila wanapopita hakuna walichofanikiwa zaidi ya kupigwa danadana.

"Tumehangaika vya kutosha bila majibu hadi leo hii kuja hapa kwa waandishi wa habari ili kutoa kilio chetu kwa viongoz,i wakuu wa nchi kuwaomba kusikia kilio chetu hiki cha muda mrefu kwani siyo sisi wapo askari wengi nchini na wengine wamekufa bila kupata haki zao. "Mimi hapa hata kutoka kwenye nyumba ya shirika nimeshindwa familia zetu zinapata shida, hadi sasa nadai Sh. milioni 16, nimekwenda mara nyingi kwa mhasibu mkuu wa TRC bila mafanikio. Tunaomba Rais atusaidie tupate haki zetu," alisema.

Meneja Mstaafu wa Jeshi hilo, Enock Mpilimi, alisema amefanya kazi katika kikosi hicho kwa miaka 34 na kwa mara ya mwisho kulipwa fedha hizo ni mwaka 2013.

Alisema, wakiwa kazini kabla ya kustaafu walikuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kusindikiza treni za mizigo bila malipo yoyote ya posho za kujikimu.

"Tulikuwa tunasindikiza treni za mizigo katika mikoa mbalimbali bila hata fedha ya kula na ukiuliza unapewa adhabu, hivyo tulikuwa tunajaza madai na kuahidiwa kulipwa baada ya kutoka safari lakini hali haikuwa hivyo na mimi hadi sasa nadai Sh. milioni 12.8. tunaomba taarifa hii iende kwa Rais wetu mama Samia ili atusaidie,"alisema.

Aidha, Sajenti Mstaafu Michael Ngongi alisema, amefanya kazi katika kikosi hicho kwa miaka tisa na anadai Sh. milioni 5.8 za posho ya kujikimu.

"Nimekuwa nikienda kudai lakini Mhasibu Mkuu wa TRC amekuwa akinipa majibu ya ubabaishaji kwani tayari niliwapelekea madai yangu lakini kiasi ambacho wanalipa ni kidogo sana.

"Nilikuwa na matatizo ya mgonjwa nikaenda kuomba nilipwe lakini unapofika tuu mlangoni kwa muhasibu anakwambia hapa hakuna hela,"alisema.

Pia alisema, katika madai yake ya Sh. milioni 5.8 hadi sasa kiasi ambacho anakumbuka kulipwa hakizidi Sh. milioni moja.



# Wagonjwa wa saratani waongezeka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR ina wagonjwa wapya wa saratani 124 ambao wamehudhuria kliniki kwa mwaka 2021 na saratani ya shingo ya kizazi inaongoza kuwa na wagonjwa wengi zaidi.

Hayo yalisemwa jana na ofisa wa kitengo wa maradhi yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Lulu Omar Bakari, wakati akizungumza na Nipashe mjini Zanzibar.

Alisema ugonjwa wa saratani unaongoza kwa vifo duniani kote na inakadiriwa zaidi ya vifo milioni 10 vimetokea katika mwaka 2020 wastani wa mtu mmoja kati ya watu sita.

Katika kipindi cha miaka mitatu kutoka 2019 hadi 2021, alisema Zanzibar ina wagonjwa 415 wa saratani ambao wamehudhuria katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Alisema wagonjwa hao ni wa saratani ya matiti 164, saratani ya shingo ya kizazi 149 na saratani ya tezi dume 102.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, katika idadi hiyo ya wagonjwa wa saratani 415 kutoka mwaka 2019 hadi 2021, wagonjwa 121 walifariki dunia.

Alisema saratani hiyo ya shingo ya kizazi inaongoza kwa kusababisha vifo vya wanawake wengi duniani.

"Mwaka 2019 wagonjwa waliolazwa Hospitali ya Mnazi Mmoja wanaougua saratani ya shingo ya kizazi ni 157 na waliofariki dunia ni wanane. Mwaka 2020 walikuwa 101 waliofariki dunia ni 19 na mwaka 2021 walikuwa 73 na waliofariki 33," alisema.

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2011 wa Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa kuwa asilimia 85 ya vifo vya saratani hutokea katika nchi zinazoendelea na kila mwaka zaidi ya wanawake 300,000 wanakufa kutokana na saratani ya shingo ya kizazi.

Pia alisema vichocheo vya ugonjwa wa saratani asilimia 60 yanahusishwa na mtindo wa maisha na ulaji usiofaa.

Alisema ulaji wa nyama nyekundu kupita kiasi huongeza saratani kwa asilimia 15, vyakula vya kusindika, vilivyokuzwa kwa kemikali nyingi ikiwamo mbolea, vyakula vyenye mafuta mengi na vyakula vilivyoota ukungu ni chanzo kikubwa cha kuongezeka kwa saratani.

Kichocheo kingine, alisema ni matumizi ya tumbaku na sigara na kwamba tumbaku huwa na kemikali 66 zinazofahamika kama kemikali za carcinogenic na sumu ambazo huchangia sana ongezeko la saratani za koo, mapafu, ini na matiti.

Pia alisema vichocheo vingine ni matumizi ya pombe kupita kiasi huku akiweka bayana kwamba pombe imebainika kuwa kisababishi cha wagonjwa wapya 740,000 wa saratani duniani kwa mwaka 2020. Hiyo ni kwa mujibu wa takwimu kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Saratani (IARC).

"Mionzi hatari (ionizing radiation)-ultraviolet kutoka kwenye miale ya jua na mionzi ya X-ray, uzito uliozidi kwa kutokufanya mazoezi pia ni vichochoe vya kupata saratani," alisema.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Juma Makungu Juma, kuwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwandishi wa Rais aapa kuwa DC

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mwandishi wa Habari wa Rais wa Zanzibar, Rajab Mkasaba, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja.

Mkasaba jana alikula kiapo cha kuitumikia nafasi hiyo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, kutokana na uteuzi wa baadhi ya viongozi uliofanyika hivi karibuni.

Hafla hiyo ya kiapo ilifanyika jana Ikulu Zanzibar na baada ya kula kiapo, Mkasaba aliahidi kufanya kazi kwa bidii na uwadilifu katika kuwatumikia wananchi huku akiahidi kuwa atahakikisha anamsaidia Rais katika kusimamia maendeleo endelevu.

Mkasaba alimpongeza Rais Dk Mwinyi kwa kumuamini na aliahidi atahakikisha anamsaidia hasa katika kufanya kazi na jamii.

Alisema atashirikiana na viongozi atakaowakuta akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja na taasisi zingine ili kutatua changamoto zinazoikabili wilaya hiyo.

Mkuu huyo akizungumzia vipaumbele vyake, alisema ni kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia fedha zilizotolewa na Dk. Mwinyi za uhueni ya UVIKO-19, hivyo ni lazima kuihamasisha jamii kuzitumia vizuri fedha hizo katika kuwainua kiuchumi.

Alisema eneo lingine ni sekta ya elimu kwa sababu mkoa umeweka mikakati maalum ili kuhakikisha matokeo yanakuwa mazuri kwa wanafunzi wa mkoa huo.

Pia alisema kwa kuwa yeye ni mwahabari, atahakikisha anaitumia sekta ya habari kwa kazi zake mbalimbali ili kupata elimu kupitia sekta hiyo.

Mwingine aliyeapishwa katika hafla hiyo ni Kamishna wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Dk. Maua Abeid Daftari ambaye alisema atamsadia Rais Mwinyi kama alivyosaidia marais waliopita kwa uadilifu mkubwa katika kazi hiyo nyeti na muhimu ambayo inahitaji umahiri mkubwa.

Alisema amejipanga kuhakikisha viongozi wanasema ukweli hasa katika mali wanazomiliki na kuwaomba wawe waadilifu katika kufanya kazi zao na waaminifu kwa serikali na wananchi.

Naye Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Juma Makungu Juma, alisema atahakikisha anatumia sheria, miongozo na taratibu zilizopo katika kutatua migogoro ya ardhi.

Alisema imani ya wananchi ndiyo itakayotatua migogoro kwa utaratibu mzuri ikiwa watakuwa wakweli na wawazi kwa kuwa mambo hayo ndiyo yatasaidia kupunguza changamoto zilizoko hasa katika kesi za migogoro ya ardhi.

Rashid Ali Salim naye aliapishwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo katika hafla ambayo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali.

# Waziri azuru usiku Bandari ya Malindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadil Abdullatif, juzi usiku alifanya ziara ya kushtukiza katika bandari ya Malindi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) kuangalia shughuli za operesheni zinavyoendelea.

Nadil aliambatana na viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Katibu Mkuu, Shomari Omar Shomari, na katika bandari ya Malindi, walikagua shughuli za ushushaji na upakiaji wa makontena kupitia meli zinazowasili katika bandari hiyo.

Alisema kwa sasa wizara ina mpango wa kuweka mfumo maalum wa kuimarisha utendaji kazi katika bandari hiyo ili kuondosha mlundikano wa mizigo.

Pia aliwataka watendaji katika bandari hiyo kujituma kwa bidii na serikali ina malengo ya kukuza uchumi wa nchi.

"Sisi viongozi wa wizara kwa kushirikiana tutafanya ziara wakati wowote katika maeneo haya ili kuimarisha utendaji kazi kwa wizara yetu," alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kuacha mara moja kuifanya bandari hiyo sehemu ya kuhifadhia makontena yao na kusisitiza kuwa serikali haitasita kuchukua hatua kwa mfanyabiashara atakayepuuza maagizo hayo.

Shomari kwa upande wake alisema mkakati wa serikali katika kupunguza msongamano wa makontena katika bandari ya Malindi utahamishia baadhi ya shughuli zake kufanyika katika eneo la bwawani.

Viongozi hao walieleza kuridhishwa na harakati za utoaji wa huduma na operesheni zinavyoendeshwa wakati wa usiku katika bandari hiyo na viwanja vya ndege.

**Nadil aliambatana na viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Katibu Mkuu, Shomari Omar Shomari, na katika bandari ya Malindi, walikagua shughuli za ushushaji na upakiaji wa makontena kupitia meli zinazowasili katika bandari hiyo.**



## AFANDE SELE

UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI AGOSTI 6, 2022



# KATEMBEA BILA KUTAMBAA

Ni bahati kubwa kuwa na mtoto ambaye ametembea bila ya kutambaa. Kutembea kwa mtoto ni lazima kupitie hatua mbili muhimu. Kwanza kukaa na kisha kutambaa, lakini kuna baadhi ya watoto wanapitia hatua mbili pekee ya kukaa na kutembea.

Mtoto anayetembea bila kutambaa inatafsiriwa na jamii nyingi kuwa ni mwenye bahati, alama ya ulezi uliokamilika na pia wazazi wake wanaelezwa kuwa wamefuata utaratibu sahihi wa malezi.

Msanii wa Bongo Fleva, Zuhura Othman Soud maarufu kama Zuchu, ni sawa na mtoto aliyetembea bila kutambaa, hii inatokana na umaarufu wake kuwa wa ghafla na usiofuata ngazi walizopitia wanamuziki wengine kama yeye.

Kila kukicha, Zuchu anazidi kuonyesha maajabu yake kwa kuvunja rekodi mbalimbali na kusababisha uongozi unaomsimamia kuonekana sawa na wazazi waliotoa malezi kwa usahihi na kufanya kupanda ngazi kwa haraka.

Akiwa na miaka 29, Zuchu ametawala muziki wa Afrika, na hivi karibuni ametajwa kuwa kinara kwa wasanii 10, wa kike katika nchi zilizopo chini ya Jangwa la Sahara,kuwa na wafuasi wengi wanaomfuatilia (subscribers) katika mtandao wa YouTube.

Zuchu amefikisha watu milioni 2.1, na kumuacha msanii toka Nigeria, Yemi Alade mwenye milioni mbili.

Rekodi hiyo, ni ya hivi karibuni lakini, tayari amewapiku wasanii wengi huko nyuma katika nyanja tofauti ya kimuziki na ikinogeshwa na nyimbo tamu anazozidondosha kila wakati.

Baadhi ya wachambuzi wanasema, Zuchu anatakiwa kuongeza juhudi na kujiepusha na mambo waliofanya wenzake waliomtangulia ambao wengi wameanguka kutokana na kukata tamaa.

Ameoonywa kwamba, mafanikio ya haraka mara nyingi yanaambatana na kiburi, nyodo na kujiamini kupita kiasi, hivyo hali hiyo anaweza kuepukana nayo kama atapenda kuwa msikivu na kujifunza kila siku.

BASI SAWA

## Afande Sele asimulia ya Mandonga



MWANAMUZIKI mkongwe wa Hip hop, Afande Sele amemuelezea bondia maarufu nchini, Karim Mandonga, kama mtu mwenye nguvu ya kula kiasi cha kumaliza sahani 10 za chipsi kwa wakati mmoja.

Akizungumza katika kipindi cha Planet Bongo cha East Africa Radio, Afande Sele amesema yeye anamjua vyema kutokana na huko nyuma alikuwa mmoja wa watu wa kundi la Watu Pori lilokuwa na makazi yake Morogoro.

"Mandonga alikuwa Watu Pori, nilikuaga nasafiri naye kwenye shoo tukifika hotelini anajifungia chumbani anafanya mazoezi, siyo mtu wa mitungi nyie mkiagiza bia moja yeye anaagiza chipsi mayai, kwa hiyo ukinywa bia 10 na yeye anakula chipsi sahani 10" - Afande Sele

## Simorix awanasa Weusi

MSANII nyota wa kizazi kipya anayeishi nchini Australia, Simorix The General, amerudi kivingine na wimbo Vaccine Remix, akiwawashirikisha wanamuziki wa kundi la Weusi.

Simorix The General ameliambia BT, kazi hiyo ni mwendelezo wa mpango wake wa kuliteka soko la Bongo pia kuipisha lugha ya Kiswahili nchini Australia kupitia muziki.

"Muda wowote kutoka sasa video ya Vaccine Remix itakuwa hewani, nimefurahi kuona audio imepokelewa vizuri na mashabiki kutoka kwenye mitandao yote ya kusikiliza na kupakua muziki, naamini hii ni hatua kubwa kwenye muziki wangu kufanya kazi na kundi bora la Hiphop Weusi,'" amesema Simorix.





## Kibibi anatamani viatu vya Samia

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan, kufanya vizuri katika kazi zake, sasa imewaongezea hari baadhi ya wanawake katika Nyanja ya siasa.

Miongoni mwa watu waliohamasika na kazi ya kiongozi huyo ni msanii wa filamu,Getrude Mwita, maarufu kama Kibibi, ambaye amesema ipo siku anaweza akawa na uongozi mkubwa.

"Kuitumikia Tanzania kwa namna ya kuwa kiongozi hicho kitu ninacho na nafikiria baadaye inaweza ikatokea nikaitumikia upande wa Serikali, nani anajua naweza nikaja kuwa hata Rais," amesema

# Maigizo: Siri ndani ya siri

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA hii imeficha siri nyingi sana, na kama siku itaamua iziweke bayana, basi watu wanaweza kukimbiana.

Mungu alipoweka kitu siri likuwa na maana yake, na kama binadamu angekuwa anafanya yote yanakuwa peupe, sijui angebaki nani duniani.

Ukiifutilia filamu hii 'Maigizo' utakutana na vitu ambavyo vitakufikirisha sana. Lakini ndiyo dunia ilivyo kwani huwa vinatokea kwenye jamii yetu.

Kufinya anaishi na mkewe Ashura. Kufunya ana mdogo wake Madebe Lidai, ambaye kwenye filamu ametumia jina la Mbulu.

Mbulu ni mlevi, mwizi na anaishi na kaka yake hapo hapo, huku akilipiwa kodi. Kila siku ni wizi na Kulinga na mkewe kazi yake kubwa ni kwenda kumtoa kwenye vituo vya polisi na kulipa madeni ya watu.

Ashura anamwambia mumewe amechoka kuishi na Mbulu, hivyo kama hatomuoa hapo, basi yeye atarejea kwao ili amuache na mdogo wake.

Kufinya hataki kuliona hili la mkewe kuondoka, hivyo kila siku anagombana na mdogo wake.

Mbulu naye anamtuhumu kaka yake kuwa anamsikiliza sana mkewe na ametawaliwa kiasi cha kumuona yeye kama hana maana.

Hali hiyo inamchanganya Kufunya, kwani anapata lawama pande zote mbili za mkewe na mdogo wake.

Kwenye nyumba hiyo hiyo anaishi Mwanjala na mkewe. Mkewe Sauda amekuwa na tabia ya kuaga kwenda sehemu mbalimbali na mumewe anamkubalia. Kuna siku akaaga anakwenda kwa dada yake, lakini baada ya muda dada mtu akafika pale. Hiyo ikaanza kumtia wasiwasi.

Kufinya hali ya mdogo wake ilivyodizi kuwa mbaya kwa wizi, akaamua kumfukuza nyumbani.

Mbulu akaanza kuishi kwa washikaji kwa kutangatanga, kwani hata kula sasa ikawa hali nyumbani.

Siku isiyo na jina alimfuata Mwanjala na kumwambia anataka kumpa zawadi. Lakini akamwambia hanayo pale amfuate. Akampeleka hadi sehemu wakagonga mlango. Ulipofunguka, Mwanjala hakuamini macho yake.

Ni kwamba mkewe alikuwa yupo na Kufinya. Kumbe ni hawara yale kitambo. Na Mbulu amewachoma kwa ajili ya kulipa kisasi cha kutimuliwa na kaka yake nyumbani. Kumbe alikuwa anajua siri ile.

Sauda anawekwa kikao cha kuulizwa kisa cha kutembea na mume wa mpangaji wenzake.

Akasema, wameishi na Mwanjala kwa muda mrefu bila kupata mtoto kitu ambacho kinamsumbua kwa mawifi zake, hivyo akaamua kutembea na Kufinya ili apate mtoto kwa sababu mkewe Ashura ni mjamzito.

Mama mmoja jirani akaja na kukuta zogo hilo, baada ya kuhadithiwa, akatoa siri nyingine kuwa tabia hiyo, kwani awali kumfuma Mbulu akifanya mambo yasiyofaa na shemeji yake Ashura.





## Mr Pimbi kumuinua Starshine

MWIGIZAJI na mdau wa burudani nchini Mr Pimbi, ameweka wazi lengo lake la kumuunganisha msanii Starshine kwenye lebo ya Rayvanny.

Starshine, ameliambia BT kuwa Mr Pimbi amevutiwa na ngoma yake 'Ananivuruga' na akampa ahadi ya kumkutanisha na Rayvanny.

" Kwangu mimi ni mafanikio makubwa kwa mdau kama Mr Pimbi kuupenda wimbo wangu mpaka kutaka kuniunganisha na lebo ya Rayvanny, mashabiki wanaweza kuendelea kusapoti ngoma zangu zipo kwenye mitandao ya muziki," amesema msanii huyo.

## JINI ANAVUKA BARABARA KAVAA NDALA

LEO tutaendelea na mfululizo wa makosa mbalimbali ambayo yanafanywa kwenye filamu za Kibongo na kusababisha kukosa mvuto.

Kila mmoja anaelewa kuwa filamu zinatengenezwa na hazina uhalisia. Ni watu wanafanya maigizo.

Lakini ni lazima muangaliaji anatakiwa asione makosa ya wazi ambayo ni ya waigizaji au muongozaji kiasi cha kumfanya mfuatiliaji kuona hata uvivu wa kuiangalia au kufutilia kisa kizima.

Maudhui, kisa, au stori yenyewe inaweza kuwa nzuri sana, lakini mazingira na jinsi ilivyoigizwa inamuacha mtu hoi.

Wiki iliyopita tuliweka makosa matano yanayofanywa kwenye filamu zetu, yanafanywa kimazoea na hayatakiwi kuwepo.

Nayo ni kila mlinzi lazima awe punguani, mtu alikwenda Ulaya kusoma miaka sita iliyopita anarudi na nguo zile zile, anarudi Ulaya na nguo ile ile, jini ni lazima acheke, uduni wa gereza na vituo cha polisi vichekesho ambavyo vinakosa uhalisia, na jambazi ni lazima awe na koti refu.

Yako mengi, lakini leo tutamalizia na makosa mengine matano.

**Mganga kutokuwa na nyumba**

Nadhani hii ilichukuliwa kutoka Nigeria na imeendelea kutumika hadi leo. Waganga wa kienyeji wa filamu za Kibongo hawana nyumba, sijui kwa nini. Wanachofanya filamu zote ni kuzungushia shuka au vitambaa vyekundu na vyeupe.

Kwa kawaida hapa nchini, waganga wengi wa kienyeji ni kweli wanaishi nje kabisa ya miji, vijijini ndani, lakini wanakuwa na nyumba, japo ni duni, za miti, mbavu za mbwa, inawezekana ni za makuti, lakini wanazo. Kwenye filamu zetu hatuoni hilo.

**Kutembea muda mrefu bila sababu**

Kuna wakati utaona mhusika, hasa mkuu anaonyeshwa anatembea kwa muda mrefu bila sababu yoyote.

Huu ni upotevu wa muda. Wakati mwingine hata wapenzi, wanaonyeshwa wanatembea muda mrefu, iwe kwa miguu au kwa gari, lakini kwa sababu ambazo hazina umuhimu wowote.

Hii inaonyesha kuwa filamu haina matukio mengi, ndiyo maana wanaweka dakika nyingi za matembezi ili filamu ionekane ndefu.

**Stori ya mwaka 1990, Bajaj kibao**

Kosa lingine ni wakati filamu inachezwa. Mhusika anaweza kuwa anakumbuka wakati wa udogo wao au ujana labda mwaka 1990. Yupo kwenye gari, anatembea kwa miguu, au vyovyote vile, lakini utaona kuna bajaj kibao zinapita. Unashangaa, mbona mwaka 1990 zilikuwa bado? Vitu kama hivi vinaonekana vidogo, lakini vina umuhimu sana.


Jamaa anawaza alikuwa ofisini mwaka 1970, lakini nyuma yake anaonekana ukutani anaonekana Rais wa sasa. Hivi ni vitu ambavyo vinatakiwa kufanyiwa kazi sana.

**Jini anavuka barabara kavaa yeboyebo**

Hili nalo tatizo. Hapa ni rahisi tu, anatakiwa jini au mzimu avuke barabara wakati magari hakuna kabisa. Lakini mtu anayecheza kama ni jini au mzimu, bado chini anakuwa amevaa viatu, au kandambili kitu ambacho si kweli.

Halafu akivuka mpaka aangalie huku na kule kuhakikisha hakuna gari. Kwa nini filamu isichezwe Jumapili jioni, wakati ambapo barabara zinakuwa hazina magari mengi?

**Wanapayuka kulazimisha hisia**



Ni wasanii wachache wanoonyesha hisia, lakini wengi wao hata ambao ni mastaa wanashindwa kufanya hivyo.

Kuna wakati filamu haihitaji hata kusema 'mimi daktari' au 'nimekasirika sana'. Akionekana tu mtu, unajua huyu ni daktari, akionyeshwa tu mtu usoni, utajua huyu amekasirika.

Wala haihitaji kupayuka ili kusisitiza jambo au kuonekana umechukia.



# Legend, Chris sy watarajia mtoto

MWANAMUZIKI wa Marekani, John Legend na mwandani wake Chrissy Teigen, wanatarajia kupata mtoto wa tatu.

Taarifa hiyo iliyowafurahisha wafuasi wao, ilitolewa na Teigen kupitia ukurasa wake wa Instagram juzi, akisema wanatarajio kuongeza familia siku si chache.

"Miaka michache nyuma nilikuwa na matumaini ya kusema imefikia mwisho, lakini ungana nasi nyumabi kuukaribisha moyo mpya ambao upo njiani," ameandika Teigen.



## Windy hata wewe waongopa!

MKUBWA akiumbuliwa mambo huwa mabaya, ndivyo hali hiyo inayomkuta mtarayarishaji wa vipindi vya mazungumzo, Wendy Williams, ambaye kwa sasa imekuwa gumzo kutokana na kuwa na maisha feki.

Kulingana na mtandao wa page Six, mwanamama huyo maarufu aliongopa kuwa yupo katika maisha ya ndoa, lakini ukweli uliobainika kwamba amedanganya kwani hana mume na anaishi peke yake.

Mtu wake wa karibu aliuambia mtandao huo kwamba Windy amedanganya kuwa amefunga ndoa na ofisa wa polisi wa New York, ukweli ni kwamba hakuna kitu kama hicho kilichotokea.

## Ne Yo subiri uyaone

MWIMBAJI na mtunzi wa muziki kutoka Marekani, Ne-Yo, ndoa yake inaweza kusambaratika, baada ya mke wake Crystal Renay, kujitokeza na kudai alikuwa akisaritiwa kwa muda mrefu.

Wanandoa hao wamekuwa katika sitofahamu baada ya kutolewa kwa malalamiko hayo, huku Renay akidai mume wake alikuwa akijihusisha kimapenzi na mwanamke mwingine zaidi ya miaka minane.

"Miaka minane nimekuwa nikidanganywa, kuna mwanamke tumeingia katika maisha ya pamoja na mume wangu, imekuwa kama fununu mwanamke huyo anauza mwili wake kwake kama kujilinda," ameandika Renay.





## Mwanzo Drake hamkumuelewa

WATU wengi wameshangazwa na hatua ya staa wa muziki kutoka Canada Aubrey Drake Graham, maarufu kama Drake kuamua kumuweka wazi mpenzi wake, Keshie Chante.

Drake alimtambulisha mpenzi wake huyo anayejulikana kama 'Kiki'mbele ya umati wa watu kwenye ukumbi wa Toronto History, siku ya Alhamisi usiku katika tamasha lake la All Canadian All Stars.

"Huyu anayekuja jukwaani ni mpenzi wangu wa kwanza kuwahi kuwa naye katika maisha yangu . Hadithi ya kweli, mtu ninayempenda kwa moyo wangu wote" alimaliza Drake.

Drake amekuwa akizungumzwa sana kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi, kutokana na tabia yake ya usiri kiasi ambacho hakuna mtu aliyemfahamu mpenzi wake.

## Beyonce si uombe radhi wakuelewe?

MKALI wa muziki wa Marekani, Beyoncé Knowle, anakabiliwa na shutuma kali kutokana na wimbo wake kuonekana kama tusi kwa watu wenye ulemavu wa ubongo.

Wimbo huo unaoitwa Heated uko kwenye albamu yake mpya ya Renaissance, una neno linaloonekana kama dharau kwa watu wenye matatizo ya kupooza kwa ubongo

Baadhi ya watetezi wa walemavu wameukosoa vibaya wimbo huo, na kuutaja kama haujakamilika kimaudhui kutokana na neno hilo linaelezewa kama la kutisha.



# Nani kuwa 'Festi Ledi' wa Kenya?

Na Mwandishi Wetu

IKIWA zimebaki siku nne raia wa Kenya kuingia katika vituo vya kupigia kura katika uchaguzi mkuu, kampeni zinazidi kuchanja mbuga katika maeneo mbalimbali ndani ya taifa hilo.

Katika nafasi ya juu ya urais, wagombea wanne wanapigana kufa na kupona kupata ridhaa ya kukalia kiti hicho huku vumbi likizidi kumtimka kati ya kambi mbili hasimu. Wagombea hao ni Raila Odinga kutoka muungano wa Azimio la Umoja Kenya, naibu rais William Ruto anayewania kupitia tiketi ya chama cha UDA, George Wajackoyah na David Mwaure wa chama cha Agano.

Hata hivyo, Odinga na Ruto wameonekana kukabiliana ipasavyo kwa kuwa kila mmoja anaonyesha nguvu zake za kisiasa kwa kufanya kampeni zitakazohakikisha anaingi Ikulu.

Wagombea hao wamekuwa kivutio cha maelfu ya watu kwenye mikutano yao ya mwisho ya kampeni.

Wakati watu wanazidi kuwaangazia wagombea hao, nyuma yao kuna wanawake ambao ndio wanahakikisha wagombea hao wanendelea kupambana.

Mmoja wa wagombea hao wanne endapo akishinda, kuna mwanamke ambaye atakua 'festi ledi' au mama wa taifa la Kenya kwa miaka mitano baada ya Margaret Kenyatta kuaga Ikulu ya Nairobi.

Je ni nani kati ya wanawake hawa wanne atachukua nafasi hiyo ambayo ni muhimu nchini Kenya?



### IDA ODINGA

Ni mke wa mwanasiasa mkongwe na kiongozi wa upinzani Raila Odinga.

Ida Anyango Oyoo, alizaliwa tarehe 27 Agosti, mwaka 1950, katika kaunti ya Migori Magharibi mwa Kenya.

Mwanamke huyo asiye na maneno mengi, alikutana kwa mara ya kwanza na Raila Amollo Odinga alipokuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Harusi yao ilifanyika Septemba 1, 1973 na katika ndoa yao walijaaliwa watoto wanne, ambao ni Fidel Odinga, Winnie Odinga, Raila Odinga Jr na Rosemary Odinga.





Kitaaluma mama Odinga ni mwalimu, lakini anasifika kuwa mwanaharakati na mfanyabiashara mkubwa.

Lakini, umaarufu wake zaidi umetokana na jinsi anavyosimama kidete katika harakati za kumuunga mkono mume wake Odinga katika siasa na azma yake ya kuongoza taifa la Kenya.

Kwa miaka mingi, amekuwa akijihusisha katika miradi tofauti ikiwamo kampeni dhidi ya uelewa kuhusu saratani ya matiti na fistula.

Pia, amekuwa mshauri wa wanafunzi kadhaa wa kike na pia mdhamini mkubwa katika kujenga maktaba ya kisasa katika shule yake ya zamani ya sekondari.

Mwaka 2021, alipewa tuzo ya kutambua uungaji mkono wake katika masuala ya afya, elimu, wanawake, amani, pamoja na uwezeshwaji wa watoto wavulana na wasichana.

### RACHEL RUTO

Rachel Chebet Ruto ni mke wa Naibu wa Rais wa Kenya William Ruto.

Alizaliwa Novemba 20 mwaka 1968 mjini Kakamega magharibi mwa Kenya. Akiishi hapo alipata masomo yake ya msingi na sekondari katika shule ya wasichana ya Butere.

Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Kenyatta na kusomea shahada ya Elimu.

Rachel na Ruto walikutana mwanzoni mwa miaka ya tisini na wawili hao walianza kuchumbiana wakiwa chuo kikuu.

Alifunga pingu za maisha na mume wake na kuanza familia yao mwaka 1991.

Rachel alijaaliwa watoto sita, wanawake watatu na wavulana watatu, mkubwa wao anaitwa Nick Ruto.

Amekuwa mstari wa mbele kupigania haki za wanawake na harakati za kuwawezesha katika jamii.

### ANNA NGIBUINI MWAURENNE MWAURE

Anna Ngibuini Mwaure ni mke wa mgombea wa urais wa chama cha Agano, David Mwaura Waihiga.

Mengi hayajulikani kuhusu maisha yake kwa sababu ameishi maisha ya ukimya, na ni nadra sana kumpata kwenye mijadala ya umma.

Mnamo Juni 2021, alikula kiapo kama jaji wa Mahakama ya Ajira na Mahusiano ya Kazi.

Uteuzi wake ulijiri wakati ambapo Rais Uhuru Kenyatta alichapisha kwenye gazeti rasmi la serikali majaji 34 na kuondoa sita waliopendekezwa na Tume ya Huduma za Mahakama.

Kabla ya uteuzi wake kama jaji alifanya kazi kama mpatanishi.

Katika taarifa zilizopita zilizochapishwa katika vyombo vya habari nchini humo, Anne amekuwa mtetezi mkali wa kutumia mbinu ya upatanishi wa mizozo baina ya wahusika bila kuwaingiza wengine.

Alibainisha kuwa njia hii ni nzuri na gharama nafuu kuliko kesi za madai.

### LEE CHEATHAM

Chatham ni mke wa mgombea urais George Wajackoyah.

Hakuna anayemjua vizuri mwanamke huyo, lakini taarifa zilizopatikana mtandaoni nchini Kenya zinaonyesha kwamba aliwahi kufanya kazi katika tasnia ya usafiri wa anga.

Alionekana hadharani siku za hivi karibuni akiwa na mume wake wakati wa mdahalo wa wagombea wa urais ambao Wajackoyah hakushiriki licha ya kufika katika eneo la tukio na kisha kuondoka.

Katika mahojiano kupitia vyombo vya habari nchini humo, Wajackoyah alisema mke wake anaishi Marekani na watoto wao watatu.



TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vituko vya shule za bweni zamani

## ●Kuiba mahindi ya walimu, wali kutia kwenye pasi ya mkaa

**Na Adam Fungamwango**



BAADA ya makala ya wiki iliyopita iliyohusiana na vibaka kutoka kupora saa, mikufu na vitambaa vya kichwani hadi simu za 'tachi', kuna mdau mmoja kwenye mitandao yetu ya kijamii alichokoza mada ya vituko vya shule za bweni ili ipatikane makala ya wiki hii.

Na kweli watu wakafunguka kweli kweli, na kuwa burudani tosha. Watu walikumbuka mbali sana. Kila mmoja alikumbuka kivyake.

Ambao waliosoma shule za day', yaani unakwenda na kurudi nyumbani kuanzia shule za sekondari wakabaki wanashangaa na kuona ajabu tu.

Wale waliokuwa wanasoma shule za bweni walikutana na vituko vingi. Wengine walifanya mambo mengi ambayo kwa sasa imebaki simulizi.

Kwenye makala haya, sitoandika mengi, bali nitakuwa stori zao wanazosimulia wenyewe jinsi walivyofanya, waliyoyakuta na yaliowakuta. Ni vituko tu na burudani ya aina yake kwa upande mwingine.

Kama kawaida, kwa sababu wengi wao kwa sasa ni watu wazima, wenye familia na baadhi kuwa na nyadhifa kadhaa serikalini na kwenye taasisi mbalimbali, huwa hawapendi majina yao yawekwe hadharani.

Wa kwanza yeye alidai kukumbuka mambo saba.

"Kuchajia simu kwenye dari la bweni, nilipokuwa nasoma shule ya Sekondari Meatu, kuficha ubwabwa, kujisaidia kwenye vyoo vya 'stafu', kujisaidia kwenye vichaka vya pembeni ya shule, kusomea kitandani, kuiba madaftari mapya ya wanafunzi wengine na kujifunika, kumwaga maji kwenye vitanda vya 'wanoko' wakati wa usiku."

Mwanafunzi mwingine wa zamani yeye alikuwa na stori yake ya kusikitisha.

"Ilikua asubuhi sana nikiwa nina kama siku tatu tangu nimeingia bweni kidato cha kwanza pale Pugu Sekondari, niliamka zangu asubuhi na mapema kujiandaa, ghafla kaja jamaa mmoja mrefu mweusi, akiwa na fagio la kudekia mbele lina kama nyavu hivi akanimbia 'dogo "niwekee dawa kwenye mswaki wangu.' Wakati huo akalinyanyulia lile dekio na kuongeza 'unashangaa nini huu ndio mswaki kidato cha nne shika weka dawa, naenda nje nikirudi nikute tayari.' Nikaogopa sana punde si punde akaja mwanafunzi mwingine na kuniambia kuwa ananitisha hakuna lolote nisiogope, na kweli jamaa yule hakurudi."

Kuna mmoja anakumbuka jinsi aliyokuwa anakwenda jikoni na kuiba wali, lakini staili yake ilikuwa ni ya aina yake.

"Nilikuwa nakwenda jikoni na pasi ya mkaa, naiba wali naushindilia kwenye hiyo pasi, we acha tu."

Kuna aliyesema kuwa, yeye anachokumbuka ni kukata magodoro ya viranja ambao ni wanoko.

"Aisee nakumbuka wahuni siku ya ugali walikuwa hawataki kuosha madishi, sasa ikifika siku ya wali nilikuwa naiba dishi anakwenda nalo bwenini." Mdau mmoja akabainisha.

Mwingine akasimuliwa jinsi alivyokutana na mwafunzi mwenzake kikojozi.

"Nakumbuka jamaa kawahi kitanda cha juu mimi cha chini, kumbe alikuwa kikojozi siku ya kwanza kakojoa kitandani, ukadondokea kitandani kwangu mimi nikadhani ni maji, asubuhi nilivyobaini, ilibidi nimshauri ashuke chini mimi nilale kitanda cha juu jamaa hakukubali, siku nyingine akakojoa tena, ilibidi nimripoti, unajua tena shule niliyosoma ilikuwa inamilikiwa na wanajeshi, jamaa kashushiwa kipigo na akalazimishwa siku hiyo alale kitanda cha cnini."

Yupo aliyekumbuka kuogeshwa maji ya mtoni na watemi, au wajuba.

"Shuleni pale palikuwa na mto usiokauka maji mwaka mzima, basi wajuba walikuwa wanakuja usiku wa manane tukiwa tumelala, wanakubeba hivyo hivyo ulivyolala, wanakupeleka mtoni, wanakulazimisha uzame mzima mzima. Kisha wanakurudisha bwenini na kukuamrisha upande kitandani kama ulivyo."

Wanafunzi wengine kazi yao ilikuwa ni kuiba mahindi ya walimu usiku kama mmoja alivyojisema.

"Mimi nakumbuka kuiba mahindi ya walimu usiku na kuchemsha juu ya dari, mchana kugoma kula sababu ya chakula kibaya."

Yupo aliyekumbuka wakati wa michezo ya shule za sekondari UMISETA.

"Nakumbuka tulicheza mechi na shule moja ya mchanganyiko tukawafunga na madawati yao tukayabeba kupeleka shuleni kwetu kulikuwa na uhaba wa madawati, lakini tukaipata."

Halafu kuna aliyekumbuka zile mechi za madarasa kwa madarasa, wakitoka huko ni ugomvi tu.

Kulikuwa pia na mambo ya kutishana.

"Kuna kitu tulikuwa tunaita 'ambushi', mwalimu akija usiku. Ukisikia hivyo unakimbia. Wanafunzi pamoja na utani, kwenye hili swala hatukuwa tunataniana." Mdau mwingine akamjibu.

"Nimecheka sana, mtataniana vyote ila kwenye ambushi' lazima heshima iwepo."

Mdau mmoja ambaye hakusoma shule za bweni, baada ya kufuatilia stori za wanazopita wenzake akaandika.

"Kumbe ambao hatukusoma shule za mabweni tulikosa uhondo."

Mama mmoja ambaye wakati huo alikuwa msichana tu, aliguswa na akaandika.

"Nilikuwa nadeka sana nyumbani, lakini nakumbuka mama alikuwa ananiambia kuna maisha maisha magumu duniani, we deka tu nikawa naona kama ananiongopea. Nilipoingia kidato cha kwanza nikapelekwa shule ya bweni.

Sikuwahi kula maharage magumu ya aina ile, tena wakati mwingine unakuta mengine yana wadudu, ugali mgumu, dona na wakati mwingine kande la mahagare yale yale, wadudu juu, ikikuwa ikifika jioni nalia sana, nakumbuka nyumbani. Nakumbuka mama alivyokuwa ananiambia, nilikonda sana. Lakini nilipozoea, yaani niliona kawaida tu."

**Tuma meseji 0716 350534**



## HABARI KIMATAIFA

### China yarusha ndege 20 Taiwan, Marekani yalalama yadai uchokozi

**WASHINGTON,** Marekani

BAADA ya China kurusha ndege zake za kivita zenye makombora ndani ya kisiwa cha Taiwan, Serikali ya Marekani imezungumza kuhusu mazoezi ya kijeshi ya nchi hiyo kuwa hayana uhalali na yenye athari.

Nchi hiyo inaendelea kufanya mazoezi karibu na Taiwan kwa siku tatu mfululizo na jana ilirusha ndege hizo zilizoingia katika mstari wa mpaka kati ya china na kisiwa hicho ambacho inadai ni sehemu yake.

"Hatua ya kijeshi ya China ni kubwa, ina athari, na bila uhalali wowote inasababisha mgogoro," alisema Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken.

Alisisitiza kwa kusema mazoezi hayo hayana uhalali kwa matendo yao. Kauli hiyo aliitoa Blinken, wakati akizungumza katika mkutano wa Asia.

China ilijibu kwa kufanya mazoezi hayo kufuatia ziara iliyofanywa juzi nchini Taiwan na Spika wa Baraza la Wawakilishi la Marekani, Nancy Pelosi.

Ziara hiyo ambayo serikali ya China ilikuwa imeonya kwa muda mrefu kwa kusema itachukua hatua ya kushangaza.

Marekani pia ilimuita balozi wa China nchini humo, Qin Gang, katika Ikulu ya nchi hiyo kutaka maelezo kuhusu suala hilo, hayo kulingana na gazeti la Washington Post.

"Kufuatia hatua za China, tumemwita Balozi Qin Gang kwenye Ikulu ya White House kuelezea vitendo vya uchochezi vya PRC [Jamhuri ya Watu wa Uchina]," msemaji wa Ikulu ya Marekani John Kirby aliliambia gazeti hilo.

Hatua hiyo, inachukuliwa kama maandamano ya kidiplomasia.

Kirby aliongeza kuwa utawala wa Biden umekosoa hatua za kijeshi za China, mbazo ni kutowajibika dhidi ya lengo leo la muda mrefu la kudumisha amani na utulivu katika Mlango Bahari wa Taiwan.

**CHINA ZARUSHA NDEGE**

Ndege za kivita za China jana zilikuwa zikiruka juu ya kisiwa cha Pingtan cha bara ambacho kiko katika Mlango-Bahari wa Taiwan kutoka kaskazini. Eneo hilo mojawapo ya sehemu iliyo karibu zaidi katika bara na kisiwa hicho.

Picha zilionyesha ndege hizo zikiruka zikiwa na makombora.

Watalii katika kisiwa hicho walikuwa wakiziona ndege hizo kwa kutumia darubini.

China pia ilirusha makombora juu ya Taiwan kutoka Kisiwa cha Pingtan siku ya Alhamisi.

Kama tulivyoripoti hapo awali, wizara ya ulinzi ya Taiwan ilisema kwamba meli na ndege nyingi za China zimevuka mstari wa kati wa Taiwan Strait kwa siku ya pili mfululizo. **BBC**



Mkazi wa kitongoji cha Johannesburg akikimbia baada ya kuibuka ghasia zilizosababisha wageni kulengwa na kuchomewa nyumba zao moto jana. **PICHA: BBC**

# Kampeni za lala salama leo

- Odinga, Ruto kuitikisa Nairobi
- Kila mmoja awania 51% ya kura zote

**NAIROBI,** Kenya

WAKATI zimebaki siku tatu wananchi wa Kenya kuamua nani atakuwa rais wao, mikutano ya kampeni inafikia tamati leo.

Kwa muda wiki nzima wagombea wamekuwa katika harakati za dakika za lala salama kutafuta kura kwa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Juhudi kubwa zimeonekana kufanywa kwa kwa kambi za wagombea kutafuta mbinu za kuwavutia wapiga kura ambao hadi sasa bado hawajaamua nani watampatia kura zao.

Kulingana na sheria za Kenya, leo saa 12 jioni ndiyo siku ya mwisho ya kampeni ya mikutano yote ya kisiasa.

Wagombea wanne wa urais nchini humo wametoa ratiba ya mikutano yao ya mwisho ya kampeni zao za mwisho.


Mpaka jana kura za maoni zimeonyesha kwamba wapiga kura ambao hawajaamua mgombea gani wa urais watampigia kura ni kati ya asilimia 6 hadi 8 ya watu wote wenye haki ya kupiga kura na kuandikishwa.

Akizungumza na kituo kimoja cha runinga cha nchini humo, mtafiti na mchambuzi wa kura za maoni Tom Wolf, alieleza kwamba, katika muda huu mfupi uliosalia, wagombea wanaangalia maeneo ambayo yana ushawishi mkubwa, na palipo na wapiga kura wengi.

"Kunaweza kuwa na eneo ambalo kuna uungwaji mkono mkubwa lakini hakuna wapiga kura wengi. Kwa hiyo tunataka kuwekeza haya masaa na siku muhimu zilizosalia zinapiganiwa maeneo yenye wapiga kura wengi," alisema Wolf.

Aliongeza "kazi nyingine ni jinsi ya kuangalia data ya namna watu walipiga kura katika chaguzi tatu au nne zilizopita."

> **Nimekuja hapa leo (jana), kuwaambia nyinyi watu wangu ya kwamba ninataka mjitokeze kwa asilimia mia wakati huu. Tusipoteze hata kura moja. Walio wagonjwa hospitalini nendeni mkawachukue wapelekeni wapige kura kisha muwarejeshe wodini.**



Raila Odinga



Naibu Rais William Ruto

**RUTO KUREJEA NAKURU**

Naibu Rais William Ruto jana alirejea jijini Nakuru baada ya kukamilisha mikutano katika maeneo ya Mlima Kenya ya Laikipia na Nyandarua.

Leo muungano wake wa Kenya Kwanza unatarajiwa kukamilisha kampeni zake mjini Narok na Nairobi. Aliyekuwa makamu wa Rais Musalia Mudavadi ambaye pia ni mfuasi wake alielezea imani yake kuhusu matokeo mazuri kwenye uchaguzi wa wiki ijayo.

Kiongozi wa Muungano wa Azimio la Umoja Raila Odinga, alimalizia kufanya mikutano yake ya kampeni maeneo ya Lamu, Malindi na Mombasa.

Odinga anahitimisha kwa kufanya mkutano mkubwa wa kampeni Jijini Nairobi alikopangiwa kufanya katika uwanja wa Kasarani.

Akizungumza katika eneo la Nyanza linaloaminika kuwa ngome yake, Raila aliwataka wapiga kura kujitokeza kwa wingi katika mkutano wa leo.

"Nimekuja hapa leo (jana), kuwaambia nyinyi watu wangu ya kwamba ninataka mjitokeze kwa asilimia mia wakati huu. Tusipoteze hata kura moja. Walio wagonjwa hospitalini nendeni mkawachukue wapeleke ni wapige kura kisha muwarejeshe wodini. Walio na ulemavu wasaidiwe wapige kura, hakuna kulala," alisisitiza Raila.

George Wajackoyah mgombea wa urais kupitia tiketi ya chama cha Roots, alipangiwa kufanya kampeni yake eneo la magharibi na kumalizia mikutano yake jijini Nairobi. Naye David Mwaure mgombea wa chama cha Agano atahitimishia mikutano yake jijini Nairobi.

Kulingana na tume ya IEBC waliosajiliwa kupiga kura ni watu milioni 22, na 122,532, ambao ni pamoja na idadi ya wapiga kura 10,443 walio ughaibuni. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RUKWARO OTHNIEL SENKORO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN PATHFINDER** yenye usajili namba **T143 DCR , CHASSIS NAMBA: VSKJVWR51Z0498245** na **ENGINE NAMBA: YD25795657B.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/311565/2022**

## AFFIDAVIT OF DISCREPANCY DATE /YEAR BIRTH

**I RAYMUNDA SIMON MGAYA** ,Tanzania ,Adult ,resident of Moshi Urban, Kilimanjaro Region,with Mobale No 0783830265, Do hereby Sworn and state as follow:

1. That , I was born on **1st JANUARY 1975** and this is the date appeared in my Certificate of birth as well.
2. That upon printing my citizen Identity card they inadvertently and erroneously written my date /year of birth as **1st JANUARY 1972** instead of **1st JANUARY 1975.**
3. That,I am executing this Affidavit of discrepancy attest to the truth of the foregoing in the fats and explain this discrepancy as regard to my dates/ year of birth.

**VERIFICATION:**
**I RAYMUNDA SIMON MGAYA** , being the deponent herein verify that all what is stated in the paragraph 1,2 and 3 here in above are true to the best of my knowledge .

Verified at Moshi this 18 day of July 2022

**RAYMRUNDA**
**DEPONENT**

**SWORN** at Moshi by the said
**RAYMUNDA SIMON MGAYA**
Who is known to me personally/
Identified to me by –
Who is known to me personally,
In my presence this 18 Day of
July 2022

**RAYMUNDA**
**DEPONENT**



**BEFORE ME**
Name **GLORY JOSEPH TAIRO**
Signature ..............................
**Date 18 July 2022**
Qualification: **COMMISSIONER FOR OATHS**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMANNE RAMADHANI MTENDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **(FUSO-MITSUBISHI)** yenye namba za usajili **T 396 DNH**

Chassis namba: **FK628K540188**

Injini namba : **6D17920043**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MKB/RB/IRI/135/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MAOMBI MADOGO**
**MADAI YA ARDHI 07 YA 2021**
**ISMAIL MOHAMED...................... 1 MDAI**
**SHABANI ALLY KIBWANA......... 2 MDAI**
**SALMA ALLY.............................. 3 MDAI**
**DHIDI YA**
**NURDIN KIGULUHUNA....................... 1 MDAIWA**
**ERASTO E NGOWI................................ 2 MDAIWA**
**DISMAS A MAGELE.............................. 3 MDAIWA**

### WITO WA MAHAKAMA

KWA: ERASTO E. NGOWI – MDAIWA 2
DISMAS A. MAGELE –MDAIWA 3

Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu, ambayo imepangwa kutajwa tarehe 11 mwezi wa 08 mwaka 2022 saa 03:00 asubuhi mbele ya mheshimiwa jaji P.J. Ngwembe.
Mnatakiwa kuhudhuria nyie binafsi au mawakili au mtu yeyote aliyeadhinishwa kusimama kwa niaba yenu na pia mnatakiwa kutoa maelezo yenu siku hiyo na nakala zote za ushahidi utakazo tumia kwa shauri hili.
**Zingatieni** kwamba, kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu, mahakama itaendelea kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wenu.
Imetolewa chini ya muhuri wa mahakama kuu kanda ya Morogoro leo siku ya tarehe 01 mwezi wa 08 mwaka 2022

**NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU**
**MOROGORO**

---

**THE LAND REGISTRATION ACT {CAP334}**
**LOSS OF CERTIFICATE OF TITLE**

**TITLE NUMBER** 3033-MBYLR

**RESTERED OWNERS;** SPAIDA MWAJENJE OF P.O.BOX258 MBEYA
**APPLICANT;** RAHABU NKOFU MUHENGA OF P.O.BOX258 MBEYA
**LAND;** L.O.N.O.124665, Plot NO.627,BlockQ Mwanjelwa Area,Mbeya city.
**AREA;** 5000,Square feet.

**TAKE NOTICE** that certificate of Title to the land decribed above is said to be lost and that I intend to issue a new certificate of Title in lieu theof unless cause to the contrary is shown within one month from the date this notice is published in the official Gazette. The orginal certificate of Title if found should be delivered to the principal Assistant Registra of Titles, Land Regstry, P.O.Box 2984, Mbeya.

S.I.Diombanya
IT.REGISTI

**S.I. Diombanya**
**ASSISTANT REGISTRAR OF TITLES**
**REGIONAL- MBEYA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA NJOMBE**
**KITUO CHA NJOMBE MJINI**
**MKOA NJOMBE**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA 57/ 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**JOHN CHALAMILA MNG'ONG'O MAREHEMU WA MTWANGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA**
**JOHN MN'ONG'O MWOMBAJI**

### TANGAZO KWA UMMA

**(KANUNI YA 5(2) YA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MIRATHI MAHAKAMA ZA MWANZO)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 mwezi 08 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
**Imetolewa leo tarehe 03 mwezi 8 mwaka 2022**

HAKIMU MKAZI

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **SAVERA XAVERY NDWANO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Sanya yenye namba za usajili **T 374 CKY,** injini namba **1621MJ410600689** na chassis namba **LKIPCKLI4B1100071.** Ameto taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/307612/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0621430163.**

---

**UNCLE MO ENTERPRISES**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya udalali ya **UNCLE MO ENTERPRISES** kwa mamlaka iliyopewa na Mahakama ya Tanzania inatangaza nnada wa hadhara utakaofanyika tarehe 18/08/2022 kuanzia saa nne kamili asubuhi katika maeneo NALA MZANI- Dodoma. MNADA HUO NI WA KUUZA SUKARI TANI 55.25 MALI YA NDUGU 1. SAMO ALLY ISAACK 2. MWINYI RAMADHANI MAGWIRA 3. PETER KITIWA 4. REGINAL LOGISTICS LIMITED 5. ILOVO SUGAR KIGALI LIMITED

**MAWASILIANO**
**0717417520,**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NA.60/2022**
**DEOGRATIAS ELENIUS MTITU::::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.AKIBA COMMERCIAL BANK::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**2.BARAZA PAUL DABAVUNJE:::::::::::::::::::::MDAIWA**
**3.JOHARI YUDA MAHENGE::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**4.ZAINABU JUNUS:::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**

### YAH:KUITWA SHAURINI

**KWA: BARAZA PAUL DABAVUNJE NA, ZAINABU JUNUS**

Fahamu kwamba **DEOGRATIAS ELENIUS MTITU** amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa **tarehe 11/08/2022 saa 2:30** asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere mwenyekiti wa baraza.Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Msipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo nyie kuwepo.
**Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 28/07/2022.**

...........................
**T.MUNZERERE**
**MWENYEKITI**
**28/07/2022**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO;114/2021**
**ANASIA A.CHILAMBO[Msimamizi wa mirathi]**
**Marehemu ALBERT CHILAMBO....................MDAI**
**DHIDI YA**
**1;OSCAR CHILAMBO..................MDAIWA**
**2;BENSON aka BEYCESON AMON.............................MDAIWA**
**3;ZAWADI CHUNGU...............................MDAIWA**

### YAH; KUITWA SHAURINI

**KWA;**
**OSCAR CHILAMBO,BENSON aka BEYCESON AMON,NA ZAWADI CHUNGU**

Fahamu kwamba **ANASIA ALBERT CHILAMBO** amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kusomwa hukumu **tarehe 25/08/2022** mchana mbele ya Mh.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Mnatakiwa kufika kwa ajili ya kusomewa hukumu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya .
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka;Msipohudhuria siku hiyo baraza`litasoma hukumu ya kesi hiyo pasipo nyie kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa baraza`hili leo **tarehe 27/7/2022.**

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**27/07/2022**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO**
**USIKOSE GAZETI**
**LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HADITHI**

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji.

## Kama ipo, ipo tu-**17**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani.

Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

****************************************

"Unajua, mimi nataka sana dada yangu aolewe, amepata tabu sana hapa kwenye hiki kijiji, tena kama akitoka hapa na kwenda kwingine itakuwa vizuri sana, ila sijui anakwenda wapi na huyo mwanaume ni nani na atamtunza vipi." Dibwela alieleza wasiwasi wake.

"Usiwe na wasiwasi kaka, kama dada yako akikubali, utamuona huyo shemeji yako, siyo mtu mbaya, tumekwambia anaishi Chalinze, ni bosi wetu. Siyo kwamba ana pesa sana, hapana, ila kama uwezo wa kumtunza dada yako anao sana tu." Daudi akamtoa wasiwasi.

"Tungeweza kuja naye, lakini si unajua mila, tena za Kiafrika, tumeleta barua, tuje na mhusika, hapana. Sisi tumeelekezwa tuje hapa kama washenga, nyinyi ndiyo mtapanga siku ya yeye kuja kujitambulisha." Akadakia Billy.

***********************************

"Haya dada, hawa nao wamekuja kwa nia ile ile kama ya yule wa kijiji cha jirani. Wameleta barua ya posa." Dibwela alimpasha dada yake, baada ya kuingia ndani na kuanza kuongea kwa faragha.

Alipofika tu baada ya kusalimiana na wageni, kaka yake alimwita ndani kumweleza ni kitu gani wageni hao walikifuata pale.

"Wametoka wapi?"

"Chalinze. Wameniambia kuwa wao ni washenga tu, na wameleta barua, huyo mchumba mwenyewe ameelezwa kila kitu chako, na hana wasiwasi na wewe, anachotaka ni kukuoa tu."




"Kaambiwa na nani?" Siwatu akauliza.

"Hilo sijui, lakini huyo mchumba sifa zako na kila kitu ameelezwa tayari kwa hiyo hana tatizo kabisa, ni wewe tu ridhaa yako."

Kwa mara ya kwaza Siwatu kuna kitu kilimwambia akubali. Alimkataa Maiko na barua iliyokuja kutoka kijiji cha jirani, lakini safari hii aliona akubali tu.

Kwanza, alichoka na mambo yanayoendelea hapo. Aliona akiolewa na kuondoka ataondokana na ombwe baya lililomkuta kwenye kijiji hicho kwa mwaka mzima.

Amekuwa kwenye matatizo mengi ya kutengwa, kunyanyaswa na pia kubakwa, hivyo alionekana kuchoshwa na maisha ya hapo.

"Kaka si utabaki peke yako?" Akajikuta anaropoka.

Dibwela aliona kama sasa dada yake anaonekana kubadili mawazo yake. Huenda akakubali.

"Hakuna shida, mashamba yote na nyumba hizi za kwako, mimi nitazisimamia vizuri tu, usiniangushe dada yangu, kubali tu."

"Sawa, pokea kwanza barua yao, halafu mengine tutaongea baadaye."

Jibu hilo lilionekana kama ni ushindi mkubwa kwa Dibwela. Lakini akashangaa kuona dada yake safari hii amekubali kirahisi zaidi, tena kwa mtu ambaye hamfahamu na wala hajawahi kumtia machoni.

Dibwela alitoka na kuendelea na mazungumzo na wageni, huku Siwatu akiaga na kuondoka kwa sababu tayari alikuwa amekamilisha kazi yake.

"Amekubali barua ipokelewe." Dibwela aliwajibu wageni hao na baada ya hapo furaha ikatawala upande wao.

"Wiki ijayo mje kupokea majibu, na baada ya hapo mchumba mwenyewe anatakiwa kuja kujitambulisha." Akawakumbusha wageni hao.

************************************

Kijiji kizima kilipata taarifa kuwa Siwatu ameposwa na sasa amekubali. Waliokasirika walikasirika, waliofurahi sawa, na walioona wivu nao walikuwamo pia.

Kila mmoja aliongea lake. Wengine wakidai hata akiolewa hawezi kukaa na mume kwa sababu ana kiburi, anadeka kwa sababu alizaliwa peke yake kwa baba na mama yake, ambao walifariki na kijiji kikamlea kwa kumdekeza kwa kipindi kirefu hadi kilipomgeuzia kibao.

Tayari walioleta barua ya posa, walikuwa wamerudi wiki moja baadaye kuchukua majibu.

Majibu yalikuwa mazuri, kwani Siwatu alikubali, na kwenye barua ya majibu kiliwekwa mpaka kiasi cha mahari.

Kilichosuburiwa ni mchumba kufika kujitambulisha. Hata hivyo Daudi na Billy, walitoa taarifa kuwa mchumba alikuwa amesafiri kidogo, hivyo wangefika naye pale wiki jayo na si hiyo.

Kabla yote hayo hayajafanyika, kijiji kilipokea mgeni mwingine. Mgeni huyu aliwashangaza wanakijiji wengi. Hakuwa mgeni kijijini hapo. Ni Bakari. Yule kijana aliyeokolewa na Siwatu kwenye msitu baada ya kukutwa akiwa nusu hai nusu mfu baada ya kupigwa na kutupwa na watu wasijulikana.

Siwatu hakuamini macho yake. "Waooo Bakari." Akainuka na kwenda kumkumbatia kwa nguvu kiasi cha bado kidogo waanguke.

"Oooh, Siwatu wangu, nimekukuta salama, siamini." Yalikuwa maneno ya Bakari wakiwa wamekumbatiana, kila mmoja akiwa na hisia kali.

Machozi yalimtoka Siwatu. Hakuamini alichokiona. Alikuwa amekaa kwenye mlango wa nyumba yake akifikiria mambo mbalimbali. Kwa mbali alimuona mtu anakuja. Moyo ukampasuka ghafla kwa sababu jinsi alivyo na utembeaji ni kama mtu anayemfahamu sana.

Kila hatua aliyokuwa anapiga mtu yule, ndivyo alivyozidi kuvutika kumuangalia zaidi. Ndipo alipogundua kuwa aliyekuwa akakaribia nyumbani kwake, si mwingine ila ni Bakari.

"Umekuja kama ulivyoahidi, siamini, siamini. Nilijua umekwenda moja kwa moja." "Haiwezekani Siwatu, nilikwambia nitarudi. Ila tu sikujua nitarudi baada ya muda gani."

"Ila umechelewa sana Bakari, mimi nilijua baada ya miezi mitatu au ikizidi sita, mwaka sasa umeniacha mkiwa." Akalalamika Siwatu huku machozi yakimtoka. Alikuwa anazungumza kwa sauti kama ya mtoto anayemdekea mama yake ambaye hajamuona kutwa nzima na amenyimwa chakula.

"Samahani, na pole sana mkombozi wangu. Ila nimerudi, nimekuja kukuona."

Kitu ambacho kilimshangaza Siwatu, ni kwamba Bakari aliyeondoka pale mwaka mmoja uliopita, na yule aliyekuja pale walikuwa ni kama wawili tofauti.

Yule aliyelazimisha atolewe porini akiwa na majeraha ya vipigo, na kulazimika kupewa nguo na Dibwela, akila chakula kwa msaada wa Siwatu kwa miezi mitatu, hakuwa yule tena.

Alikuwa amenawiri, amevaa nguo za gharama, ndiyo maana hata Siwatu alishindwa kumfahamu mapema.

Walishikana mikono kama wapenzi waliopotezana kwa muda mrefu, wakaingia ndani, kila mmoja akiwa na furaha tele, akitaka kujua nini kilitokea baada ya kutoonana machoni kwa mwaka mzima.

Kesho yake Siwatu alimsimulia kile kilichotokea pale. Kuanzia kubakwa na mtu asiyejulikana, kuokota leso chini ya kitanda ambayo ilidaiwa kuwa ni ya kijana mmoja kijijini hapo aitwaye Maiko, na hata uongozi wa kijiji kumtuhumu yeye ndiye aliyefanya kitendo hicho.

Siwatu na Bakari hawafichani kitu japo hawakuwahi kuwa wapenzi, alimfahamisha pia mpaka jinsi ambavyo ameposwa.

"Mhh umepata mchumba?"

"We acha tu, nimekataa barua za wachumba wawili. Hii ya tatu nimeshindwa mwenzangu, maana wewe ulivyokuwa hapa, kidogo ulikuwa unanipa kampani, hata wakinizodoa nina wewe, leo hii haupo, nimekuwa mpweke sana, nimekomaa weee, mpaka nimeamua kusalimu amri, nimekubali kuolewa." Siwatu akajibu akimtazama Bakari usoni.

**Walishikana mikono kama wapenzi waliopotezana kwa muda mrefu, wakaingia ndani, kila mmoja akiwa na furaha tele, akitaka kujua nini kilitokea baada ya kutoonana machoni kwa mwaka mzima.**

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# PLUIJM, KASEKE WATEMA CHECHE SINGIDA BIG STARS

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van der Pluijm akiwataka wachezaji wake kuacha kucheza kistaa na badala yake wapambane kwa sababu ya ugumu uliopo katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, mfungaji wa bao pekee, Deus Kaseke amewataka mashabiki wa timu hiyo kuwa na subira.

**Singida Big Stars ilitambulisha kikosi chake katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Zanaco kutoka Zambia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Liti, Singida juzi.**

Katika mechi hiyo maalum kwa ajili ya kukitambulisha kikosi kipya kwa mashabiki wa nyumbani, ambapo mbali na wachezaji wengi kutambulishwa, kivutio kikubwa kilikuwa ni Meddie Kagere aliyejiunga akitokea Simba.

"Tumetengeneza nafasi tatu za kufunga mabao hatukuzutumia hasa kipindi cha pili, tulikuwa kuna wakati tupo mchezoni, lakini kuna kipindi tunapotea. Kwa nafasi zile zilitakiwa ziwe mabao, haitakiwi tucheze kama wanafunzi na kama tunataka kupambana na timu kubwa za hapa nchini basi kila mechi kwetu iwe fainali, soka ni kama vita, usipomuua mwenzako atakuua wewe.

Hatutakiwi tucheze kwa sababu tuna wachezaji wenye majina makubwa, tunatakiwa tuwe pia na ari ya kupambana," alisema Pluijm kocha wa zamani wa Yanga na Azam.

Pluijm alisema amefurahi kurejea tena Tanzania na anaamini ataipa matokeo chanya timu hiyo iliyomwani na kumpa jukumu la kuinoa.

"Nimejisikia raha, nimerudi nyumbani na kufunga. Hapa Singida kwangu ni kama nyumbani tu, ila kwa sasa tunaomba mashabiki wetu watuvumilie kwa sababu wachezaji wengi ni wapya, kocha bado hajapata muunganiko, tumecheza kwa asilimia sabini tu ya uwezo wetu," alisema Kaseke.

Naye beki aliyejiunga na timu hiyo akitokea Simba, Paschal Wawa, alisema amefurahi kujiunga na Singida Big Stars na kwa sababu wamempa nafasi nyingine ya kudhihirisha uwezo wake.

"Hapa nimekuja kufanya kazi, sikuja kufuata upendo, nimeacha timu kubwa, nimekuja kwenye timu hii nayo ni kubwa, ni nafasi ya kuonyesha na kudhihirisha uwezo wetu," alisema Wawa.



Baadhi ya mashabiki wa Yanga wakiwa katika foleni ya uchangiaji damu ambalo limefanyika sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya kuelekea katika Wiki ya Mwananchi inayohitimishwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taifa Queens yapania makubwa

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Timu ya Netiboli ya Taifa (Taifa Queens), inatarajia kuondoka nchini Agosti 16, mwaka huu kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Afrika, nyota wa timu hiyo, Dawa Vuai ametamba wamejipanga kwenda kufanya vyema katika michuano hiyo.

Mashindano ya netiboli ya Afrika yamepangwa kufanyika kuanzia Agosti 20 hadi 28, mwaka huu katika Mji wa Pretoria.

Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Devotha Marwa, aliliambia gazeti hili kambi ya timu hiyo inaendelea vizuri na maandalizi ya safari yako kwenye hatua za mwisho.

"Mungu akipenda timu itaondoka Agosti 16, mwaka huu, tumejipanga kwenda kushindana, tumedhamiria kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania," alisema Marwa.

Naye nyota wa timu hiyo, Vuai alisema wamejipanga vizuri kuelekea katika mashindano hayo na lengo lao kubwa ni kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

"Tumejipanga kwenda kushindana na si kushiriki, tunaendelea vizuri na mazoezi hapa kambini kwetu, tunaipongeza CHANETA kwa namna walivyojipanga," alisema Vuai.

## Aliyeweka rekodi asajiliwa Kagera

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa kwanza kufunga bao katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita akiwa na Mbeya Kwanza, Edgar William amejiunga na Kagera Sugar.

Taarifa iliyotolewa na Kagera Sugar jana imesema mchezaji huyo amepewa mkataba wa miaka miwili na wana imani anatoa mchango mzuri kwenye kikosi chao.

William alifunga bao pekee katika mechi ya kwanza ya msimu uliopita iliyochezwa saa nane mchana, kati ya Mbeya Kwanza dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Nyota huyo anakuwa mchezaji wa sita kutua Kagera Sugar iliyodhamiria kurekebisha mapungufu yake na kurejea katika ushindani kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Wachezaji wengine waliosajiliwa na Kagera Sugar ni Anuary Jabir kutoka Dodoma Jiji, Laurent Alfred (Azam FC), Abdulaziz Makame (Namungo FC) na Datius Peter kutoka Polisi Tanzania.

## Kundemba yatamba kuimaliza KMKM FC

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Kundemba FC, Nadir Kijo amesema timu yake iko imara na anaamini ataibuka na ushindi katika mechi ya mashindano ya Pre Season dhidi ya KMKM itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Kundemba imepata nafasi ya kushiriki mashindano hayo maalumu ya kuziandaa timu kuelekea katika msimu mpya wa 2022/2023 baada ya Chipukizi kujitoa.

Kijo aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari na mchezo huo na amepanga kutumia wachezaji wake wote waliosajiliwa ili kufahamu mapungufu na ubora wa kikosi chake kabla ya kuanza kwa ligi.

Alisema anafahamu anakutana na timu yenye uzoefu katika ligi na mashindano mbalimbali lakiniamewaandaa wachezaji wake kuongeza utulivu na umakini ili kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo.

"Tunajua uwezo wa KMKM lakini katika ushindani lazima mmoja ashinde, unaweza kushinda kwa kusonga mbele lakini pia unaweza kushindwa na kupata kile ulichokihitaji kutoka kwa wachezaji wako"alisema Kijo.

## ZISIKUPITE

### BARCA KUMUUZA AUBAMEYANG

BARCELONA wako tayari kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye umri wa miaka 33 kwenda Chelsea. (***Mirror***)

### LEICESTER YAIGOMEA CHELSEA

OMBI la Chelsea la kutaka kumnunua mlinzi wa Leicester, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21 kwa pauni milioni 60 limekataliwa. (***Mail***)

### ADAMS ANUKIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imeanza mazungumzo na Southampton kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Scotland, Che Adams mwenye umri wa miaka 26. (***Football Insider***)

### GIBBS-WHITE SOKONI

KLABU ya Nottningham Forest pia wanavutiwa na kiungo wa kati wa Wolves, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 22. (***Sky Sports***)

### UDOGIE AKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wanakaribia kufikia makubaliano ya pauni milioni 21 ya kumnunua beki wa kushoto wa Udinese ya Italia mwenye umri wa miaka 19, Destiny Udogie. (***Telegraph***)

### CORNET, WEST HAM SAFI

MAXWEL Cornet wa Burnley mwenye umri wa miaka 25 anatazamiwa kufanyiwa uchunguzi wa afya kule West Ham baada ya kufikia kipengele cha kumnunua winga huyo wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast kwa dau la pauni milioni 17.5. (***Mail***)

### UNITED YAKATA TAMAA

KLABU ya Manchester United iko tayari kujiondoa kwenye vita ya kuwania saini ya kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25 dhidi ya Chelsea 25. (***Mirror***)

### TORREIRA KUTUA GALATASARAY

LUCAS Torreira amekubali kujiunga na Galatasaray, ambayo itailipa Arsenal kati ya dau la pauni milioni tano au sita ili kumnunua kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Uruguay mwenye umri wa miaka 26. (***Fabrizio Romano***)

### DEPAY ATAKIWA JUVE

KLABU ya Juventus imeonyesha nia ya kumsajili fowadi wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 kutoka Barcelona. (***Sport***)

### GOUIRI ANUKIA MADRID

REAL Madrid inatumaini klabu ya Nice itapunguza thamani yao ya euro milioni 40 kwa Amine Gouiri ili kumsajili mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, kwa nia ya kusalia na timu hiyo ya Ufaransa kwa mkopo msimu huu. (***Sport***)

### GALTIER KUSAJILI WATATU

KOCHA mpya wa Paris St-Germain, Christophe Galtier anatumaini kusajili wachezaji wengine watatu baada ya kiungo wa kati wa Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 24 kujiunga nao akitokea Lille na kuwa mchezaji wao wa nne kusajiliwa majira ya joto. (***Sport***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND: SIHOFII KUNG'ARA ENGLAND

**Mshambuliaji huyo asema ni suala la muda makali yake kuanza kuonekana...**

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Erling Haaland anasisitiza 'hana wasiwasi' kuhusu kung'ara katika Ligi Kuu England baada ya mechi ngumu ya kwanza dhidi ya Liverpool kwenye Ngao ya Jamii.

Akiwa na Darwin Nunez kwenye kikosi cha Liverpool, mchezo huo ulichukuliwa kuwa wa vita kati ya washambuliaji nyota wapya wa ligi hiyo.

Lakini Haaland alitoka katika nafasi ya pili bora, akikosa nafasi kubwa huku Nunez akiweka jina lake kwenye ukurasa wa mabao katika ushindi wa Liverpool.

Gwiji wa City, Sergio Aguero baadaye alikiri raia huyo wa Norway alipewa wakati mgumu na Virgil van Dijk na 'amezoea sana' kucheza Ujerumani.

**Haaland aliwasili katika soka la England akiwa na mabao 134 katika mechi 137 alizocheza kwa klabu na nchi tangu kuanza kwa msimu wa 2019/20. Lakini sasa hii ndiyo changamoto yake ngumu zaidi.**

"Watu wanaweza kuchukua muda, watu wanaweza kuja moja kwa moja ndani yake. Tunapaswa kuona, lakini sina wasiwasi. Hayo ni maisha kama mwanasoka - lazima uishi nayo," alisema mchezaji huyo akiambia Sky Sports.

"Naweza kuboresha kila kitu," alisema. "Ikiwa unafikiri mimi ni mzuri katika jambo moja, ninaweza kuwa bora kila wakati.

"Hili ni jambo ninalopaswa kufanya. Nikiwa mchezaji mchanga, nikicheza chini ya Pep Guardiola, nikichezea katika klabu bora zaidi ya England, sina budi kuendelea kujiendeleza na kuwa bora katika mambo mengi.

"Hilo ndilo ninalopenda sana kuhusu soka, unaweza kuendeleza kila wakati, unaweza kuwa bora zaidi kwenye mchezo."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,019,3

MECHI KALI
EVERTON
VERSUS
CHELSEA
1 | 5.20
X | 3.75
2 | 1.61

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AZPILICUETA AIKATAA BARCELONA



**LONDON,** England

CESAR Azpilicueta ameweka rasmi mustakabali wake Chelsea kwa kusaini mkataba mpya wa miaka miwili hadi msimu wa joto wa mwaka 2024.

Azpilicueta alikuwa na nia ya kujiunga na Barcelona ili kutafuta changamoto mpya mapema msimu huu wa joto, lakini amechagua kuongeza muda wake wa kukaa pale Stamford Bridge kwa jumla ya miaka 10.

"Nina furaha sana kuongeza muda wangu wa kukaa Chelsea, nyumbani kwangu," alisema nahodha huyo wa Blues.

"Ni takriban miaka 10 tangu nilipowasili na kujiunga na klabu hii, kwa hiyo ninahisi upendo na ninafurahi sana kwa mradi mpya tulio nao mikononi mwetu."

Azpilicueta alitoa shukrani maalum kwa mmiliki mpya, Todd Boehly na mmiliki mwenza Behdad Eghbali kwa fursa ya kuendelea.

"Ningependa kusema asante kwa Todd na Behdad kwa kunipa fursa ya kuendelea na safari yangu katika klabu hii ya ajabu na ninatazamia kwa hamu kuendelea na safari yetu.

"Mimi ni nahodha wa fahari sana na ninatumaini tunaweza kushiriki kumbukumbu nyingi nzuri pamoja," alisema.



# Konate kukosa mwanzo wa msimu

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imethibitisha, Ibrahima Konate, amepata jeraha ambalo litamweka nje ya uwanja mwanzoni mwa msimu wa Ligi Kuu England 2022/2023.

Beki huyo alisajiliwa msimu uliopita wa joto kwa dau la pauni milioni 36 na akawa kiungo muhimu wa kikosi cha Wekundu hao, akicheza mechi 29 katika mashindano yote huku klabu hiyo ikishinda mataji mara mbili.

Konate sasa anatazamiwa kukosa kuanza kwa kampeni yake ya pili kama mchezaji wa Liverpool kutokana na kuumia.

Taarifa rasmi kutoka kwa klab hiyo kuhusu jeraha hilo ilisem "Ibrahima Konate anatazamiv kukosa kuanza kwa msimu v 2022-23 baada ya kupata jeral wakati wa mechi ya Jumapili kujiandaa na msimu mpya dhidi RC Strasbourg Alsace.

"Beki wetu wa kati alilazimi kutoka uwanjani katika kipindi cl pili cha pambano la Anfield baad ya kupata goli."

Beki huyo aliandika kwen mtandao wake wa kijamii akisem "Kwa bahati mbaya, natakiwa k kaa nje ya uwanja, lakini si mu mrefu sana. Kwa sasa, nitafan kila niwezalo kurejea."

HABARI MICHEZO

301,493/-

# AZAM FC YAHAMIA CAIRO KUSAKA MECHI ZA KIRAFIKI

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC kimeondoka katika mji wa El Gouna kuelekea Cairo ili kusaka mechi nyingine za kirafiki na timu kubwa kwa ajili ya kumpa nafasi kocha kufanya tathmini ya kikosi baada ya mazoezi ya wiki mbili yanayoendelea huko nchini Misri.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia 'Zaka', alisema Kocha wao, Abdihamid Moallin amefanya kazi kubwa kuitengeneza timu hiyo na sasa anataka aangalie matokeo yake kwa kuhitaji mechi dhidi ya klabu kongwe tofauti na zile walizocheza awali.

"Wiki ya kwanza (kocha) alikuwa na kazi ya kuitengeneza safu ya ulinzi, iliyofuata akaanza kusuka mastraika na sasa anataka angalau mechi mbili kubwa na siyo zile ambazo tumecheza. Mfano tuliyocheza nayo Grand FC tukashinda bao 1-0 ni ya Daraja la Pili, kwa hiyo tunatoka El Gouna na kwenda Cairo kusaka mechi angalau mbili kabla ya kurejea nyumbani," alisema Zaka.

Ofisa huyo alisema endapo itashindakana kupata mechi hata moja, tayari wamefanya mipango ya kucheza mchezo na timu kutoka Kuwait na baada ya hapo kocha atajua kikosi chake kilipofikia.

Azam imeweka kambi yake Misri kwa ajili ya kujiandaa na michuano mbalimbali, ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA, Kombe la Mapinduzi na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mpaka sasa kikosi hicho kimecheza mechi mbili tangu ambapo ya kwanza ilikuwa ni dhidi ya Wadi Degla ya huko na kuchapwa bao 1-0 huku mchezo wake wa pili ikishinda goli 1-0 dhidi ya Grand FC, mfungaji akiwa ni Mzimbabwe Prince Dube.

Azam FC itafungua pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara Agosti 17, mwaka huu kwa kuwakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.




Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni wakijiandaa na mechi ya marudiano dhidi ya Malawi kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika (BSAFCON) itakayochezwa kesho kwenye fukwe ya Coco jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanesco, NHIF zaanza vyema

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Tanesco imeichapa Chui mabao 3-1 katika mechi ya kwanza ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa ya Wavu iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

Mechi nyingine za ligi hiyo zilizochezwa ni kati ya NHIF iliyoifunga Nyika mabao 3-1 wakati Faru na Serengeti walitoka sare ya 3-3 sawa na Hazina iliyopambana na Kigamboni huku Kampala University ikiwaacha hoi Jeshi Stars kwa kuwafunga mabao 3-0.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena leo kwa UDSM kuvaana na KIUT wakati Jeshi Stars itawakabili NHIF, Magereza wao watachuana na Mafinga Parish na Satar Girls itawakaribisha Golden Wings, mechi zote za wanawake.

Wakati huo huo, Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu katika Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Alex Mkenyenge amewataka wachezaji na waamuzi kuzingatia nidhamu pamoja na kufuata sheria za mchezo huo ili kupata bingwa sahihi.

Mkenyenge alisema hayo katika uzinduzi rasmi wa ligi hiyo na kuongeza kwa kufanya hivyo, mchezo huo utakuwa na atapatikana bingwa imara.

"Nawashukuru Chama cha Mpira wa Wavu kwa namna walivyojiandaa na kuhakikisha haya yanafanyika, ningeomba viongozi, wachezaji na waamuzi kuzingatia sheria na nidhamu katika mashindano haya kwa sababu ndio msingi wa ukuaji wa mchezo husika," Mkenyenge alisema.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/22 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.29 | 3.29 | 3.09 |
| 02. 06/08/22 | 17:00 | Bristol City vs Sunderland | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 03. 06/08/22 | 17:00 | QPR vs Middlesbrough | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 04. 06/08/22 | 17:00 | Reading vs Cardiff | 2.44 | 3.18 | 2.94 |
| 05. 06/08/22 | 17:00 | Swansea vs Blackburn | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 06. 06/08/22 | 17:00 | Burton vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.33 | 2.88 |
| 07. 06/08/22 | 17:00 | Charlton vs Derby | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 08. 06/08/22 | 17:00 | Exeter vs Port Vale | 2.53 | 3.17 | 2.82 |
| 09. 06/08/22 | 17:00 | Fleetwood Town vs Plymouth | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 10. 06/08/22 | 17:00 | MK Dons vs Sheffield Wed | 2.61 | 3.21 | 2.71 |
| 11. 06/08/22 | 17:00 | Shrewsbury vs Accrington | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 12. 06/08/22 | 17:00 | Barrow vs Bradford City | 2.59 | 3.13 | 2.78 |
| 13. 06/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 14. 06/08/22 | 17:00 | Hartlepool vs AFC Wimbledon | 2.89 | 3.24 | 2.44 |
| 15. 06/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 16. 06/08/22 | 18:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 17. 06/08/22 | 21:30 | Hansa vs Arminia Bielefeld | 2.64 | 3.34 | 2.59 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 06 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1182 | Norwich City vs Wigan | 1.63 | 3.54 | 5.38 |
| 14:30 | 1785 | Fulham vs Liverpool | 9.57 | 5.78 | 1.25 |
| 15:00 | 2744 | Ural Yekaterinburg vs Spartak Moscow | 4.29 | 3.60 | 1.76 |
| 16:30 | 1755 | VfL Bochum vs Mainz | 3.04 | 3.34 | 2.21 |
| 16:30 | 2498 | VfL Wolfsburg vs Werder Bremen | 1.83 | 3.65 | 3.85 |
| 16:30 | 2999 | Augsburg vs SC Freiburg | 3.20 | 3.40 | 2.11 |
| 16:30 | 4997 | Monchengladbach vs Hoffenheim | 2.08 | 3.91 | 2.91 |
| 16:30 | 5347 | Union Berlin vs Hertha BSC | 1.73 | 3.61 | 4.41 |
| 17:00 | 1003 | Bournemouth vs Aston Villa | 3.55 | 3.35 | 2.00 |
| 17:00 | 1083 | Tottenham vs Southampton | 1.34 | 4.99 | 7.58 |
| 17:00 | 1143 | Ross County vs Celtic | 11.09 | 6.05 | 1.22 |
| 17:00 | 2203 | Stoke City vs Blackpool | 2.07 | 3.25 | 3.45 |
| 17:00 | 2295 | Aberdeen vs St Mirren | 1.99 | 3.26 | 3.76 |
| 17:00 | 2591 | Bristol City vs Sunderland | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 17:00 | 3248 | Sheffield Utd vs Millwall | 1.82 | 3.35 | 4.30 |
| 17:00 | 3562 | Nordsjalland vs Viborg FF | 2.23 | 3.46 | 2.96 |
| 17:00 | 3983 | Preston vs Hull City | 1.93 | 3.35 | 3.80 |
| 17:00 | 4247 | Reading vs Cardiff | 2.45 | 3.10 | 2.85 |
| 17:00 | 4278 | Newcastle vs Nottingham | 1.62 | 3.69 | 5.18 |
| 17:00 | 4672 | QPR vs Middlesbrough | 2.94 | 3.19 | 2.34 |
| 17:00 | 4768 | Leeds vs Wolverhampton | 2.24 | 3.26 | 3.06 |
| 17:00 | 4996 | Burnley vs Luton Town | 1.75 | 3.55 | 4.40 |
| 17:00 | 5346 | Rangers vs Kilmarnock | 1.22 | 5.84 | 12.08 |
| 17:30 | 1685 | Fortuna Sittard vs Ajax | 11.03 | 6.62 | 1.19 |
| 17:30 | 4222 | CSKA Moscow vs Fakel | 1.44 | 4.39 | 6.39 |
| 17:30 | 4884 | Rio Ave vs FC Vizela | 2.32 | 3.16 | 3.06 |
| 18:00 | 1300 | Josko Ried vs Sturm Graz | 3.10 | 3.34 | 2.09 |
| 18:00 | 2197 | Wolfsberger AC vs LASK Linz | 2.75 | 3.39 | 2.26 |
| 18:00 | 4641 | Strasbourg vs Monaco | 2.57 | 3.22 | 2.67 |
| 18:45 | 5240 | Pisa vs Brescia | 2.70 | 3.20 | 2.55 |
| 19:00 | 1613 | Spezia vs Como | 1.61 | 3.92 | 5.03 |
| 19:15 | 2818 | Charleroi vs Oostende | 1.60 | 3.96 | 5.01 |
| 19:15 | 3912 | Sivasspor vs Gaziantep BB | 2.02 | 3.47 | 3.42 |
| 19:30 | 3653 | Everton vs Chelsea | 5.20 | 3.75 | 1.61 |
| 19:30 | 4170 | Borussia Dortmund vs Bayer Leverkusen | 2.01 | 3.94 | 3.04 |
| 19:30 | 4491 | Farco FC vs Ismaily SC | 3.56 | 2.76 | 2.32 |
| 19:45 | 4408 | Cambuur vs SBV Excelsior | 1.88 | 3.65 | 3.65 |
| 20:00 | 1449 | FC Krasnodar vs Lokomotiv Moscow | 2.40 | 3.50 | 2.65 |
| 20:00 | 3989 | Akhmat Grozny vs Zenit St Petersburg | 4.80 | 4.00 | 1.61 |
| 20:00 | 5844 | GD Estoril vs Famalicao | 2.50 | 3.12 | 2.82 |
| 20:30 | 4348 | TSV Hartberg vs RB Salzburg | 8.06 | 5.51 | 1.26 |
| 21:00 | 3387 | PSV Eindhoven vs Emmen | 1.18 | 6.57 | 11.95 |
| 21:30 | 4486 | Grasshoppers vs St. Gallen | 2.65 | 3.55 | 2.40 |
| 21:45 | 5128 | Besiktas vs Kayserispor | 1.51 | 4.23 | 5.64 |
| 22:00 | 1018 | Empoli vs Spal | 1.66 | 3.77 | 4.83 |
| 22:00 | 2849 | Pyramids vs Arab Contractors | 1.47 | 4.10 | 6.60 |
| 22:00 | 3307 | Clermont Foot vs Paris St Germain | 8.80 | 5.68 | 1.27 |
| 22:00 | 3445 | Waalwick vs Utrecht | 3.56 | 3.51 | 1.95 |
| 22:15 | 3434 | Torino vs Palermo | 1.54 | 4.03 | 5.64 |
| 22:30 | 2429 | Porto vs Maritimo | 1.19 | 6.43 | 13.07 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Agosti 6, 2022

Nipashe




## Haaland: Sihofii kung'ara England

UKURASA 21




Rais wa Yanga, Hersi Said (kushoto) na Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi wakiwa wameshikilia nakala za mkataba baada ya Mtunisia huyo kusaini mkataba mpya wa kuendelea kukinoa kikosi hicho cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: YANGA SC**

# Yanga: Siku yetu

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

## Nabi rasmi aongeza miaka 2 Jangwani huku Pitso akiwanoa...

IMEWADIA. Kilele cha siku iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu na mashabiki na wanachama wa Yanga maarufu Wiki ya Mwananchi imefika huku mabosi wa klabu hiyo wakimtambulisha mmoja wa wageni wao ni aliyekuwa Kocha Mkuu wa Al Ahly ya Misri, Pitso Mosimane.

**Ukiondoa utambulisho wa wachezaji watakaoitumikia Yanga katika msimu mpya wa 2022/2023, siku hiyo itapambwa na burudani mbalimbali na kuhitimishwa kwa mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Vipers FC kutoka Uganda.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Pitso aliipongeza Yanga kwa kutwaa makombe matatu katika msimu uliopita na kusema amefurahi kuwa sehemu ya sherehe za klabu hiyo zitakazofanyika leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Nimefurahi kupata mwaliko kuja Tanzania kuungana na timu ya Yanga katika kuadhimisha Wiki yao ya Mwananchi, niliwahi kufika hapa nchini mara nne, nilifikia Zanzibar lakini sikupata nafasi ya kuangalia timu za Tanzania," alisema Pitso.

Kocha huyo nguli alisema kwake imekuwa ni faraja kutembelea sehemu za historia zilizopo Makumbusho ya Taifa ambapo aliona kumbukumbu za viongozi walioshiriki kuhakikisha mataifa ya Afrika yanapata Uhuru.

Aliongeza lengo la yeye kuja hapa nchini ni kuungana na timu hiyo katika kuendesha programu ya watoto ambayo itasaidia kuendeleza vipaji.

"Tulishangaa kuona mapokezi ambayo yalifanywa na Watanzania pamoja na mashabiki wa Yanga wakati timu hii ilipopata ubingwa, kiuweli imeweka historia," aliongeza kocha huyo.

Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said, alisema ujio wa kocha huyo ni mwendelezo wa kuadhimisha kilele cha Wiki ya Mwananchi ambayo itamalizika leo.

"Tumefurahi kujumuika na kocha mwenye mafanikio barani Afrika, tunaamini kupitia yeye ataitangaza vizuri Tanzania katika tasnia ya michezo," alisema Hersi.

Rais huyo alisema ujio huo unaonyesha jinsi mpira wa Afrika unavyozidi kukua siku hadi siku na kuongeza unawasaidia baadhi ya vijana kupata ajira.

Kuhusu mechi dhidi ya Vipers, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ambaye jana alisaini mkataba mpya wa miaka miwili alisema atautumia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi ya mechi ya Ngao ya Jamii watakayocheza dhidi ya Simba.

Nabi alisema katika mchezo huo atawakosa nyota wake wawili, Jesus Moloko na Lazarous Kambole ambao waliumia katika mechi ya kirafiki iliyopita ambayo walicheza dhidi ya Namungo.

"Nimeridhika na viwango vya wachezaji wangu, lakini kuna kazi kubwa ya kufanya kwa ajili ya msimu mpya ili kuhakikisha tunatetea mataji yetu, tukianza na Ngao ya Jamii ambayo tutacheza dhidi ya Simba, ni mchezo mgumu na utakuwa wenye ushindani kwa sababu ya uimara wa wapinzani wetu,"alisema Nabi.

# Dalali aipeleka Simba Day CAF

**Na Hadija Mngwai**

WAKATI uongozi wa Simba ukikiri kuchelewa kutambulishwa kwa jezi mpya ni tatizo, aliyekuwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Dalali amesema Tamasha la Simba Day kwa sasa limekuwa ni tukio la kimataifa barani Afrika tofauti na lilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuwa watulivu na wakae tayari kuzipata jezi mpya kabla ya Tamasha la Simba Day halijafanyika.

Ahmed alisema sababu kubwa iliyopelekea jezi kuchelewa ni mazungumzo ya kupata mdhamini mpya, lakini akasema jezi hizo ziko njiani.

Naye Dalali aliliambia gazeti hili jana kwa sasa maandalizi ya Simba Day yamekuwa makubwa na kupongeza weledi unaofanywa na viongozi walioko madarakani.

"Simba ya sasa sio ile ya mwanzo, viongozi wanaendeleza vyema tamasha hili, Simba Day ya kwanza ilifanyika mwaka 2009 na lengo lilikuwa kukusanya pesa kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo ya klabu ambapo tulipata Sh. milioni 70, kiasi kidogo kilitumika kupata Uwanja wa Bunju," alisema Dalali.

Aliongeza anafurahi kuona viongozi wamefanya usajili bora na mechi za kirafiki zilizochezwa zitakuwa zimesaidia kuimarisha kikosi huku akiamini wataurudisha ubingwa wa ligi waliopokonywa na watani zao.

Kilele cha Simba Day kinatarajiwa kufikia keshokutwa ambapo mbali na zoezi la kutambulisha wachezaji wapya, timu yao itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya mabingwa wa Ethiopia, St. George wakati Simba Queens itawaalika Fountain Gate Princess kutoka jijini Dodoma.

Baada ya tamasha hilo, Simba itaendelea na mazoezi yake kwa ajili ya kuwakabili Yanga katika mechi ya kuwania Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13 na Agosti 17, mwaka huu itawakaribisha Geita Gold FC kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >